



MAONI YA MPIOGACHAPA

—O—

SOMA GAZETI

LA

SERIKALI SASA

JAMHURI YA MUUNGANO
WA TANZANIA

—O—

GAZETI

KWA KUIKUZA

LUGHA YAKO

YA TAIFA

—O—

(KISWAHILI)

BEI SH. 1/25

Linatolewa kwa Idhini ya Serikali na
limeandikishwa Posta kama
Gazeti

DAR ES SALAAM

YALIYOMO

	Taarifa ya Kawaida Uk.		Taarifa ya Kawaida Uk.
Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka, n.k.	Na. 423 215	Kupotea kwa Vyeti vya Bima	Na. 451-2 231
Notice re Supplement	Na. 424 216	Uthibitisho na Usimamiaji wa Mirathi	Na. 453-4 231
Tanzania	216	Uthibitisho na Usimamizi	Na. 455 231
Kutoa Barua za Utambulisho	Na. 425-6 216	Uendeshaji wa Mirathi	Na. 456 231
Ofisi ya Bodi Kuu ya Tenda—Matangazo ya Tenda	Na. 427-8 216	Taarifa ya Mdaiwa	Na. 457 231
Matokeo ya Mthani wa Serikali wa Kutunza Hesabu	Na. 429 216	Taarifa ya Mgawanyo wa Faida	Na. 458 231
Matokeo ya Mthani wa "Office Management"	Na. 430 216	Maombi ya Leseni za Magari ya Abiria, n.k.	Na. 459 232
Baraza la Uamuzi la Wafanya Kazi—Mikataba ya Hvari	Na. 431-44 217/29	Baraza la Leseni za Usafirishaji	Na. 460 234
Ubatilisho wa Haki ya Kumiliki Ardhi	Na. 445-7 230	Makampuni Yanayotarajiwa Kufutwa katika Daftari la Makampuni	Na. 461 234
Kupotea kwa Hati ya Kumiliki Ardhi	Na. 448 230	Tangazo la Kuuza Biashara	Na. 462 234
Kupotea kwa Hati ya Kusafiria kwa Ndege	Na. 449 231	Mali Isiyo na Mwenyewe	Na. 463 234
Kupotea kwa Waranti za Kusafiria	Na. 450 231	Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa	Na. 464 235
		Hati za Fedha za Hazina	Na. 465 235

KUAJIRIWA NA KUKABIDHIWA MADARAKA

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 423

Wizara ya Tawala za Mikoa na Maendeleo Vijijini:

Kuwa Maafisa Maelezo Wasaidizi, daraja la II:—

Bibi A. TEGETE, kuanzia tarehe 3 Machi, 1970.
Bibi O. GIMBI, kuanzia tarehe 6 Aprili, 1970.
Bibi H. W. NTUNDU, kuanzia tarehe 20 Juni, 1970.
R. MATITU, kuanzia tarehe 24 Juni, 1970.
Nd. AKYOO, kuanzia tarehe 30 Juni, 1970.
Bibi M. MUTANI, kuanzia tarehe 1 Julai, 1970.
Bibi V. K. A. ALLI, kuanzia tarehe 1 Agosti, 1970.
G. MVUNGI, kuanzia tarehe 5 Septemba, 1970.
G. H. MUYUGI, kuanzia tarehe 5 Septemba, 1970.
Bibi H. MAWINGI, kuanzia tarehe 1 Januari, 1971.
J. M. MTENGERA, kuanzia tarehe 15 Machi, 1971.
Bibi G. R. MWIJUMA, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1970.
Bibi C. P. KIBWANGA, kuanzia tarehe 1 Agosti, 1970.
Bibi M. MCHONE TIMOTHY, kuanzia tarehe 1 Januari, 1971.
M. R. MODARD, kuanzia tarehe 20 Januari, 1971.
C. THOMAS, kuanzia tarehe 23 Januari, 1971.
A. K. MATAMBO, kuanzia tarehe 28 Januari, 1971.
S. S. MILINGA, kuanzia tarehe 2 Februari, 1971.
W. A. MSINGI, kuanzia tarehe 13 Februari, 1971.
M. KIMANGA, kuanzia tarehe 1 Juni, 1971.
E. A. P. MWAKYUSA, kuanzia tarehe 8 Juni, 1971.
J. M. TARIIMO, kuanzia tarehe 18 Juni, 1971.
B. R. CHIBULA, kuanzia tarehe 2 Februari, 1970.
Bibi M. MWINYIHIJA, kuanzia tarehe 1 Machi, 1970.
J. Y. ZAVALLA, kuanzia tarehe 1 Machi, 1970.
H. K. MOHAMED, kuanzia tarehe 11 Machi, 1970.
Bi. T. M. N. HASSAN, kuanzia tarehe 21 Machi, 1970.
Bi. EKONI, kuanzia tarehe 25 Machi, 1970.
Bibi E. KAPEJI, kuanzia tarehe 31 Machi, 1970.

Kuwa Maafisa Maelezo Wasaidizi, daraja la II—(inaendelea):—

Bibi T. S. MWAIPYANA, kuanzia tarehe 31 Machi, 1970.
Bi. S. KILINGO, kuanzia tarehe 31 Machi, 1970.
Bibi C. H. KISHOSHA, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1970.
Bi. L. T. BOMA, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1970.
Bi. A. BULUBA, kuanzia tarehe 1 Mei, 1970.

Wizara ya Kilimo na Vyama vya Ushirika:

Kuwa Bwana Shamba, daraja la III:—

A. J. BAGONZENKWI, kuanzia tarehe 6 Desemba, 1969.

Wizara ya Mali ya Asili na Utalii:

Kuwa Mabwana Miti, daraja la II:—

E. ATHUMANI, Bwana Miti, daraja la III, kuanzia tarehe 1 Januari, 1972.
M. H. MERO, Bwana Miti, daraja la III, kuanzia tarehe 1 Januari, 1972.
S. S. MKWAWA, Bwana Miti, daraja la III, kuanzia tarehe 1 Januari, 1972.

Kuwa Afisa wa Misitu, daraja la II:—

P. E. KIMARYO, Afisa wa Misitu, daraja la III, kuanzia tarehe 1 Januari, 1972.

Kuwa "Conservation Assistants":—

E. K. MARKI, kuanzia tarehe 1 Januari, 1971.
A. KANUNGA, kuanzia tarehe 1 Januari, 1971.
L. MARIKI, kuanzia tarehe 1 Januari, 1971.
E. LASHERI, kuanzia tarehe 1 Januari, 1971.
M. P. SYOKIMO, kuanzia tarehe 1 Januari, 1971.
M. E. SHOO, kuanzia tarehe 1 Januari, 1971.

Matangazo yahasuyo mali za watu waliofariki, kuvunja mikataba ya ushirikiano na mengineyo, yakiwa ya manufaa kwa umma; yaweza kuchapishwa katika *Gazeti*. Matangazo yote yapelekwe kwa Mhariri, Idara Kuu ya Utumishi wa Serikali, Ofisi ya Rais, S.L.P. 2483 Dar es Salaam, kabla ya Jumatatu ya kila juma. Matangazo yasitumwe kwa Mpiogachapa Mkuu wa Serikali.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 424

Notice is hereby given that Orders, as set out below, have been issued and are published in Subsidiary Legislation Supplement No. 14 to this number of the *Gazette*:—

Order under the Sales Tax Act, 1969 (Government Notice No. 53 of 1972).

Order under the Customs Tariff Act, 1969 (Government Notice No. 54 of 1972).

Order under the Customs Tariff Act, 1969 (Government Notice No. 55 of 1972).

TANZANIA

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo kilichotokea Hospitali ya Mbeya, tarehe 6 Januari, 1972 cha MOHAMED MWAPOSA, Kopro wa Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 425

FA/D. 30/3/76

KUTOA BARUA ZA UTAMBULISHO

Inatangazwa kwamba Mheshimiwa DECHO STAMBILIEV, alipokelewa na Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania saa sita na nusu (6.30) tarehe 6 Machi, 1972 huko Ikulu na alitoka barua zake za Utambulisho kama Balozi wa Jamhuri ya watu wa Bulgaria katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshima alisindikizwa na Mabwana V. TOTOROW—Trade Representative pamoja na DIMITER ROMANOV—Katibu wa tatu ambao walipata heshima ya kutambulishwa kwa Rais.

Mheshimiwa JOHN MALECELA, M.P., Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje alikuwepo.

Dar es Salaam,
7 Machi, 1972

J. F. LUGANDU,
k.n.y. Katibu Mkuu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 426

FA/D. 30/3/77

KUTOA BARUA ZA UTAMBULISHO

Inatangazwa kwamba Mheshimiwa BERNARD J. SEMALANE, alipokelewa na Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania saa saba na nusu (7.30) tarehe 6 Machi, 1972 huko Ikulu na alitoka barua zake za Utambulisho kama Balozi wa Swaziland katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa JOHN MALECELA, M.P., Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje alikuwepo.

Dar es Salaam,
7 Machi, 1972

J. F. LUGANDU,
k.n.y. Katibu Mkuu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 427

OFISI YA BODI KUU YA TENDA

TENDA NA. 4 YA 1972/73

TENDA KWA KUTAKA DALALI WA SERIKALI

1. Maombi ya tenda yanakaribishwa kwa somo lililotajwa hapo juu kwa mkataba wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 1 Mei, 1972 mpaka tarehe 30 Aprili, 1973. Kwa hapa Dar es Salaam, tu.

2. Maelezo zaidi ya tenda hii yanapatikana kwa Mwandishi, Bodi Kuu ya Tenda, S.L.P. 49, (Simu Na. 20805), Jengo la Tancot, Makao Makuu ya Mawasiliano, Dar es Salaam.

3. Tarehe ya kufungwa kwa tenda hii ni saa tatu (3) asubuhi siku ya Ijumaa, tarehe 21 Aprili, 1972.

Dar es Salaam,
2 Machi, 1972

Mwandishi,
Bodi Kuu ya Tenda

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 428

CTB/TEN/DLA/16/4

OFISI YA BODI KUU YA TENDA

TENDA NA. 55 YA 1971/72

TANGAZO LA TENDA

1. Maombi ya tenda yanakaribishwa kwa kuiuzia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vifaa vifuatavyo:—

Anaesthetic Solution, Idadi—4,000 Tins, katika 50 Catridges itolewe kwa vipindi viwili vilivyoo sawa sawa vya 2,000 Tins, katika Julai, na 2,000 Tins, katika Desemba, 1972.

2. Maelezo zaidi kuhusu tenda hii yanapatikana kutoka kwa Mwandishi, Bodi Kuu ya Tenda, S.L.P. 49, Dar es Salaam, Mawasiliano, kwa maombi.

3. Muda na siku ya kufungwa kwa tenda hii ni saa tatu (3) asubuhi tarehe 5 Mei, 1972, Ijumaa.

Dar es Salaam,
7 Machi, 1972

Mwandishi,
Bodi Kuu ya Tenda

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 429

E/CSC/4/4

MATOKEO YA MTHANI WA SERIKALI WA KUTUNZA

HESABU

NOVEMBA, 1971

MTHANI MGUMU

1. Matokeo ya mthani uliofanywa tarehe 24 na 25 Novemba, 1971 kwa mujibu wa "Establishment Circular Letter No. 4 ya 1966" ni kama ifuatavyo:—

2. Watihaniwa wafuatao wamefaulu mthani wote kwa kikao kimoja:—

Z.10 B. A. Mwashubila, Asst. Examiner of Acct. Grade I, Dar es Salaam.

Z.88 E. K. Sam, Accts. Asst., Comworks, S.L.P. 2, Tabora.

Z.92 A. M. Mwandalima, Accts. Asst., Home Affairs, S.L.P. 9223, Dar es Salaam.

3. Watihaniwa wafuatao wamefaulu somo moja waliloshindwa zamani na sasa wamefaulu mthani wote:—

Z.11 F. Byekwaso, Asst. Acct., Grade II, Education, S.L.P. 9121, Dar es Salaam.

Z.50 A. S. Lyakurwa, Accts. Asst., Treasury, S.L.P. 9111, Dar es Salaam.

Z.62 S. Singh, Accts. Asst., Police, S.L.P. 912, Dodoma.

Z.66 J. A. Karuma, Asst. Acct., Grade II, I.R.O., Iringa.

Z.67 K. R. Mbena, Asst. Acct., Grade II, Comworks, S.L.P. 23, Iringa.

Z.69 R. A. Mwakijale, Asst. Acct., Ujenzi, S.L.P. 97, Kigoma.

Z.74 E. W. Okello, Asst. Acct., Comworks, S.L.P. 81, Musoma.

Z.91 J. F. Madiwa, Asst. Acct., (Education) 37 Clerendon Road, Watford, W.D.I. IJQ., Herts, United Kingdom.

4. Watihaniwa wafuatao wamefaulu masomo mawili na kwa mujibu wa kifungu cha 15 cha "Establishment Circular No. 4 ya 1966" wanaondolewa masomo haya katika mthani wa baadaye. Masomo waliyofaulu yameonyeshwa kando ya majina yao:—

Z.15 W. A. L. J. Mwamwitwa, Acct. Asst., S.L.P. 9004, Dar es Salaam (1 na 2).

Z.26 R. E. Rwejuna, Accts. Asst., Treasury, S.L.P. 9111, Dar es Salaam (2 na 3).

Z.37 J. R. Nguluma, Accts. Asst., Police, S.L.P. 9141, Dar es Salaam (1 na 2).

Z.38 K. J. Maligana, Asst. Exam. of Accts., Exaudit, Dar es Salaam (2 na 3).

Z.71 P. M. Monasa, Accts. Asst., Comworks, S.L.P. 3051, Moshi (2 na 3).

MASOMO YA MITHANI

1=Book-Keeping and Accounts.

2=Public Finance and Administration.

3=Government Accounting.

Tume ya Utumishi Serikalini,

S.L.P. 9143,

Dar es Salaam,
7 Machi, 1972

Mangi P. I. MAREALLE,
Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 430

E/CSC/6/4

MATOKEO YA MTHANI WA "OFFICE MANAGEMENT"

NOVEMBA, 1971

1. Matokeo ya Mthani wa "Office Management" uliofanywa tarehe 24 na 25 Novemba, 1971 kwa mujibu wa "Establishment Circular Letter No. 13 ya 1965" ni kama ifuatavyo:—

2. Watihaniwa wafuatao wamefaulu mthani wote kwa kikao kimoja:—

O.9 T. K. Asenga, E.O., Immigration, S.L.P. 512, Dar es Salaam.

O.11 J. V. L. Omari, E.O., Maendeleo, S.L.P. 2248, Dar es Salaam.

O.17 A. S. Mwandiga, E.O., Treasury, S.L.P. 100, Mbeya.

O.18 J. M. Kawalege, E.O., Lands, S.L.P. 9230, Dar es Salaam.

O.19 P. M. Eponda, Diocese of Mahenge, Kwirow, S.L.P. Mahenge.

O.20 H. Nakuchema, Deputy Guide, N.S., S.L.P. 1694, Dar es Salaam.

O.22 F. M. Jonathan, E.O., Maendeleo, S.L.P. 1752, Dar es Salaam.

O.25 V. J. Mruma, E.O., Education, S.L.P. 9121, Dar es Salaam.

O.26 L. Kahana, E.O., Utumishi, S.L.P. 2483, Dar es Salaam.

O.27 L. C. Saabuni, E.O., Kilimo, S.L.P. 84, Nansio.

O.28 D. G. Kalinda, E.O., Maliasili, S.L.P. 770, Mbeya.

O.31 T. M. Kiwale, E.O., Labour, S.L.P. 9014, Dar es Salaam.

O.32 S. R. Mogella, E.O., Treasury, S.L.P. 9111, Dar es Salaam.

O.34 A. J. Haule, E.O., State House, S.L.P. 9120, Dar es Salaam.

O.43 F. C. Masiko, E.O., Tumeajiri, S.L.P. 9143, Dar es Salaam.

O.90 J. O. Makwaya, C.O., Maendeleo, S.L.P. 52, Geita.

O.48 A. Nene, Sen. Court Clerk, Judiciary, S.L.P. 3140, Arusha.

O.59 Mrs. J. R. Noronha, E.O., Utawala, Musoma.

O.63 E. M. Masawe, Typist Grade I, Maendeleo, S.L.P. 754, Mbeya.

O.81 M. A. Suleman, Sen. Court Clerk, Judiciary, S.L.P. 93, Singida.

O.82 C. R. Mulokozi, Audio-Typist, Utawala, Singida.

3. Watihaniwa wafuatao wamefaulu mthani wote kwa kurudia somo waliloshindwa hapo awali:—

O.1 A. L. Mseo, Audio-Typist, Health, S.L.P. 20500, Dar es Salaam.

O.3 N. S. Kassali, E.O., Home Affairs, S.L.P. 9223, Dar es Salaam.

O.4 B. R. Shoo, E.O., Maendeleo, S.L.P. 2676, Dar es Salaam.

O.6 E. P. Mtumbuka, E.O., Aviation Division, S.L.P. 1493, Dar es Salaam.

O.7 W. M. Saidi, E.O., Education, S.L.P. 9121, Dar es Salaam.

O.39 B. W. Nzowa, E.O., Ujima, S.L.P. 9231, Dar es Salaam.

O.49 D. R. Byabato, E.O., Utawala, S.L.P. 3050, Arusha.

O.60 C. Mutarubuka Kafumbe, E.O., Elimu, S.L.P. 54, Musoma.

O.70 N. K. Mutoka, E.O., Prisons, S.L.P. 3001, Malya.

O.71 P. M. Segeja, E.O., Kilimo, S.L.P. 1434, Mwanza.

O.73 W. M. M. Simba, H.C.O., Labour Division, S.L.P. 71, Songea.

4. Watihaniwa wafuatao wamefaulu masomo mawili na itabidi kurudia somo waliloshindwa katika mthani wa baadaye. Masomo waliyofaulu ni kama ilivyoonyeshwa kando ya majina yao:—

O.5 S. W. R. Lwasa, E.O., Bunge, S.L.P. 9133, Dar es Salaam (1 na 2).

O.15 N. B. Mkumula, E.O., N.I.R., S.L.P. 2021, Dar es Salaam (1 na 2).

O.16 A. G. Kijazi, E.O., Treasury, S.L.P. 9111, Dar es Salaam (1 na 2).

O.33 Mrs. E. A. Pokella, E.O., Utawala, S.L.P. 544, Mtwara (1 na 3).

O.41 O. M. Salimu, E.O., Tumeajiri, S.L.P. 9143, Dar es Salaam (1 na 2).

O.44 J. J. M. Salamba, E.O., Treasury, S.L.P. 9111, Dar es Salaam (1 na 3).

O.51 A. J. Nyingi, E.O., High Court, S.L.P. 943, Dodoma (2 na 3).

- O.54 F. C. Temba, E.O., Utawala, S.L.P. 3, Kigoma (1 na 2).
 O.56 S. M. A. Nachuli, E.O., Elimu, S.L.P. 725, Moshi (2 na 3).
 O.66 Miss C. M. Mbwambo, E.O., Labour, S.L.P. 183, Mtwara (2 na 3).
 O.72 Mrs. S. Masanja, E.O., Fisheries, S.L.P. 226, Mwanza (1 na 2).
 O.84 S. M. Kingaru, E.O., Kilimo, S.L.P. 26, Tabora (2 na 3).
 O.86 Tungu G. Musukula, E.O., Comworks, S.L.P. 32, Tabora (2 na 3).

MASOMO YA MITIHANI

- 1=The Structure and Organization of Government.
 2=Office Management.
 3=Stores and Accounts.

Tume ya Utumishi Serikalini,
 S.L.P. 9143,
 Dar es Salaam,
 7 Machi, 1972

Mangi P. I. MAREALLE,
 Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 431

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Hiari Na. 13 wa 1972

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

MESSRS. VEGETABLE OIL INDUSTRIES LTD., MWANZA

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkataba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA) na Messrs. Vegetable Oil Limited, Mwanza uliletwa mbele ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (a) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa.

Kibali hiki kitaanzia siku ya kwanza ya mwezi Julai, 1971.

MKATABA WA HIARI

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

MESSRS. VEGETABLE OIL INDUSTRIES LIMITED, MWANZA

1. Makubaliano:

Sisi Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika, tujulikanao hapa kwa jina "Chama" na Messrs. Vegetable Oil Industries Ltd., tujulikanao kwa jina "Tajiri" tunathibitisha hapa kwa maandishi na kutia sahihi zetu, kuonyesha kuwa, kwa uhuru na hiari yetu wenyewe tumekubaliana juu ya mambo haya yafuatayo kuhusu hali za kazi na mishahara.

2. Utambuzi:

(a) Tajiri anakitambua na kuheshimu haki za Chama, kuwa ndiye sauti na mtezezi peke yake wa wafanyakazi wote waliana wanachama wa NUTA kwa mambo yote yanayohusu hali za kazi na mishahara.

(b) Chama, kwa upande mwingine kinatambua Tajiri kuwa ndiye Muajiri peke yake wa wafanyakazi wote wanaohusika na mkataba huu.

3. Kuhusika:

(a) Mkataba huu utawahusu wanachama wote wa Chama walioajiriwa na Tajiri isipokuwa wale ambao ni wakuu wa kazi.

(b) Tafsiri ya Mkuu wa kazi:

Tafsiri ya Mkuu wa kazi itakuwa na maana ifuatayo:—

- (i) Mkuu wa Kiwanda; au
 (ii) Mkuu wa Kiwanda Msaidizi; au
 (iii) Mkuu wa Idara; au
 (iv) Mkurugenzi.

Vinginevyo, Mkuu wa kazi, ni mtu ye yote yule aliyepewa madaraka na uwezo kamili kwa maandishi wa kuajiri, kufukuza na kuachisha kazi mfanyakazi, ama uwezo wa kupendekeza juu ya kuajiri, kumfukuza, kumwachisha kazi mfanyakazi.

4. Muda na tarehe ya kuanza mkataba:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba tarehe ya kuanza mkataba huu itakuwa tarehe 1 Julai, 1971 na utaendelea kutambuliwa kwa muda usiopungua miezi kumi na mbili (12). Katika muda huu, ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkataba huu, ni lazima afuate masharti yaliyomo katika fasili ya 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal) ya mwaka 1967.

(b) Hata hivyo mkataba unaweza kuvunjwa kwa makubaliano ya pande zote mbili, lakini ye yote katika hao anayetaka kuvunja kifungu cho chote inambidi atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa mwenzake kwa ajili ya kusudio hilo.

(c) Mkataba huu utaendelea kutambuliwa wakati wote mpaka wakati huo tu ambao labda mkataba utavunjwa, au kubadilishwa au kurekebisha kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

5. Kuajiri:

Muda wa majaribio utakuwa kama ifuatavyo:—

(a) Kwa kazi zisizohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya mwezi mmoja.

(b) Kwa kazi zinazohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya miezi mitatu.

(c) Mara baada ya muda wa majaribio kumalizika mfanyakazi atahesabiwa kuwa ni mfanyakazi wa kudumu wa mwezi.

6. Uachaji au uachishwaji kazi:

(a) Katika muda wa majaribio upande wo wote:—

(i) Chini ya kifungu 5 (a) utatoa taarifa ya saa 24 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala ya taarifa hiyo.

(ii) Chini ya kifungu 5 (b) utatoa taarifa ya siku 14 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala yake.

(b) Kuhusu wafanyakazi wa kudumu, upande wo wote utatakiwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha ya mwezi mmoja badala ya taarifa hiyo. Taarifa hiyo, au malipo badala yake, ni lazima itolewe kwa maandishi.

(c) Mfanyakazi asiachishwe kazi mpaka pamekuwepo na sababu ya maana inayoambatana na uwezo au tabia yake kazini au ustawi wa kazi.

Papo hapo yafuatayo yasiwe ni sababu ya kumwachisha kazi:—

(i) Kuwa mwanachama wa Chama au kufanya shughuli za Chama nje ya saa za kazi, au wakati wa saa za kazi kwa idhini ya Tajiri au msimamizi wake wa kazi.

(ii) Kuwa mjumbe au kiongozi wa wafanyakazi au kugombea kiti cho chote cha ujumbe au uongozi wa wafanyakazi.

(iii) Kutoa malalamiko au kushiriki katika utoaji wa ushahidi juu ya Tajiri kuvunja sheria, kutokufuata Siasa ya Taifa au kufanya jambo lo lote la kuwaudhi wafanyakazi.

(iv) Ukabila, rangi, utu, dini, mawazo ya siasa na (Starehe).

7. Nafasi za kazi na upunguzaji wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kuwa, juhudi ya pamoja itafanywa ili kuongeza nafasi za kazi na kuzuia upunguzwaji wa wafanyakazi kazini, ili kusaidia Taifa katika kupambana na tatizo la ukosefu wa kazi za mishahara nchini.

(b) Hatua za kuwapunguza idadi ya wafanyakazi, zitachukuliwa tu, iwapo Tajiri atakitosheleza Chama, kuwa, hakuna uwezekano wo wote mwingine wa kuepuka au kuzuia hatua hiyo. Hizi zifuatazo zitakuwa miongoni mwa njia zifaazo kufikiriwa juu ya uepukaji wa upunguzaji wafanyakazi; uondoaji wa kazi za ziada; ubadilishaji wa wafanyakazi kutoka sehemu wasizohitajiwa na kuwaweka kwenye sehemu nyingine ambazo zitaonekana kuwa na nafasi au haja na watu hao; kutoajiri tena, kwa muda watu wapya mpaka hapo hali itakaporudia tena kuwa njema; upunguzaji wa pole pole kwa wafanyakazi wote watakoohusika.

(c) Uchaguzi wa wafanyakazi watakoohusika na upunguzwaji utafuata msingi wa "Wakwanza kuingia kazini awe wa mwisho kupunguzwa" au kufikiriwa juu ya:—

(a) Haja ya utendaji bora wa kazi za kiwanda.

(b) Uwezo, uzoovu, ujuzi na sifa za kazi za kila mfanyakazi.

(c) Muda wa utumishi.

(d) Umri.

(e) Hali ya jamii yake.

(d) Wafanyakazi ambao wameachishwa kwa ajili ya upunguzaji lazima wapewe nafasi ya kwanza ya kurudishwa kazini wakati Tajiri anapoajiri wafanyakazi wapya. Kuajiriwa tena kutafuata utaratibu uliyotaiwa hapo juu.

8. Saa za kazi:

(a) Saa za kazi zitakuwa 45 kwa juma moja. Jumapili na siku za Sikukuu kwa kawaida hakutakuwa na kazi.

(b) Kazi zote zitakazofanyika zaidi ya saa za kawaida kwa juma au kwa mwezi zitahesabiwa kuwa ni kazi za ziada ambayo lazima italipwa kwa kiasi cha 1½ (moja na nusu) ya malipo ya saa za kawaida. Ila tu, ikiwa kazi hizo zitafanyika siku ya Jumapili au Sikukuu za Kiserikali, basi malipo yake yatakuwa mara mbili ya kiasi cha malipo ya saa za kawaida.

9. Ulazima wa uanachama:

(a) Kila mfanyakazi aliyejajiriwa na Messrs. Voil Industries Ltd., atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka tarehe ya mkataba huu kutangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali.

(b) Mfanyakazi ye yote yule mpya ambaye atakayejajiriwa baada ya mkataba huu kuanza kutumika atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi 2 mara baada ya kumaliza muda wake wa majaribio. Au ikiwa hatahusika na muda wa majaribio atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka amejajiriwa.

(c) Mfanyakazi ye yote ambaye hatakuwa mwanachama wa Chama kwa mujibu wa Ibara hii atakuwa ametoa taarifa yake ya kuacha kazi.

10. Malipo ya kushikia kazi kwa muda:

Mfanyakazi anapohitajiwa na Tajiri wake kushikia kwa muda kazi yenye madaraka na mishahara Mkubwa zaidi kuliko wake na ikiwa kupitana huku kwa mishahara ni kwa kiasi kisichopungua Sh. 100/- kwa mwezi na iwapo atafanyika kazi hiyo kwa muda wa zaidi ya wiki moja, italazimu Tajiri amlipe licha ya mishahara wake wa kawaida sehemu yote ya mishahara wa kazi hiyo iliyozidi mishahara wake.

11. Nguo za kazi:

Wafanyakazi wote, isipokuwa Makarani watapata jozi 2 za nguo za kazi kwa mwaka.

Wafanyakazi wote ambao wamepewa nguo za kuhifadhi mwili itawalazimu kuzivaa katika nyakati zote za saa za kazi.

12. Ada za NUTA:

Imekubaliwa kwamba Tajiri atakuwa anakata ada za NUTA kila mwezi kutokana na mishahara wa kila mfanyakazi ambaye ni mwanachama wa NUTA na kuzituma pesa hizo katika Ofisi ya NUTA ya Mwanza.

13. Marupurupu:

Mambo yote yaliyotajwa hapa chini yatalipwa na Tajiri kwa mujibu wa "Sheria ya Marupurupu ya 1968".

(i) Likizo ya mwaka na malipo yake.

(ii) Likizo ya uzazi.

(iii) Likizo ya ugonjwa na malipo yake.

(iv) Likizo ya ugonjwa wa uzazi na malipo yake.

(v) Likizo ya dharura.

(vi) Malipo ya safari ya likizo.

14. Mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba wafanyakazi wana-stahili kupewa mafunzo zaidi juu ya kazi zao ili waweze kutoa utumishi mwingi na bora zaidi. Kwa ajili hiyo Tajiri ataweka mpango maalum wa mafunzo kwa wafanyakazi.

(b) Tajiri ataoa ruhusa bila ya kikwazo cho chote kwa mfanyakazi/wafanyakazi, wakati wa saa za kazi inapohitajiwa, ili wadhurie mafunzo ambayo mara kwa mara hutayarishwa na Chama, au Shirika lo lote la Taifa au vyyo vinginevyo.

15. Matibabu:

Tajiri ataoa cheti kwa wafanyakazi ili waweze kupata matibabu katika Hospitali ya Serikali.

16. Migogoro kazini:

(i) Migogoro yote itakayotokea kazini, kati ya Tajiri na mfanyakazi kazini ambayo inaweza kushughulikiwa chini ya Sheria ya Usalama Kazini Na. 62 ya 1964, basi sheria hiyo itatumwa kuondoa migogoro hiyo.

(ii) Migogoro au mabishano mengine ambayo hayaji chini ya Sheria Na. 62 ya Usalama Kazini ya mwaka 1964, usuluhishi wake utashughulikiwa kwanza kiwandani baina ya Kamati ya Kazi kama ipo, na Tajiri ili kufikia uelewano. Iwapo hatua hiyo haitafaulu mgogoro huo utapeleka kwa Chama kwa kufuata ngazi zake. Ikiwa bado usuluhishi haujapatikana, mgogoro huo utafuata Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi, 1967.

17. Mpango wa kukuza mazao:

Chama na muajiri wamekubaliana kwamba watawafunza wafanyakazi wote juu ya haja na faida ya kukuza utumishi bora na mengine kazini, na kuweka mipango mbali mbali itakayoonekana kuwa itafaa ya kukuza utumishi bora.

18. Posho ya safari:

(a) Ikiwa mfanyakazi atasafiri kwa muda tu kwenda kazini mahali pengine mbali ya pale mahali pake pa kawaida anapofanyia kazi atalipwa posho ya safari kama ifuatavyo:—

(i) Ikiwa safari na kazi hiyo ni kutoka asubuhi mpaka jioni, posho itakuwa Sh. 7/50.

(ii) Ikiwa safari na kazi hiyo ni kwa usiku mmoja posho itakuwa Sh. 20/-.

19. Baraza la Wafanyakazi:

Kwa vile kushirikishwa kwa wafanyakazi katika upande wa Utawala wa Kiwanda ni moja ya mambo muhimu na ya lazima, hasa kuhusu uhusiano mzuri kiwandani, kutoa ufanisi bora wa kazi na kuweka lengo la shughuli za mahali pa kazi, pande zote mbili zimekubaliana, kufuatana na kanuni zilizowekwa na Serikali kuanzisha Baraza la Wafanyakazi.

20. Nyongeza ya mishahara:

Imekubaliwa ya kwamba, nyongeza ya mishahara itakuwa kama ifuatavyo:—

Daraja la "A" Wafanyakazi 54 wanaopata mishahara kuanzia Sh. 165/- mpaka Sh. 230/- watapata nyongeza ya Sh. 30/- kila mtu kwa mwezi.

Daraja la "B" Wafanyakazi 8 wanaopata mishahara wa Sh. 231/- mpaka Sh. 350/- watapata nyongeza ya Sh. 27/- kila mtu kwa mwezi.

Daraja la "C" Wafanyakazi 5 wanaopata mishahara wa Sh. 351/- na zaidi watapata nyongeza ya Sh. 25/- kila mtu kwa mwezi.

Mkataba huu umetiwa sahihi siku ya Alhamisi, tarehe 2 Desemba, 1971.

Kwa niaba ya

Messrs. Vegetable Oil Industries Ltd.

Kwa niaba ya
Chama cha Taifa cha
Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

S. V. PATEL,
Managing Director

M. K. J. MATOKE,
Katibu wa Mkoa

B. P. DJU,
Katibu wa Tawi

M. L. EDWAR.,
Katibu Msaidizi wa Tawi

PETER MAGESA,
Mwenyekiti, Kamati ya Kazi

Dar es Salaam,
1 Februari, 1972

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 432

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Hiari Na. 216 wa 1971

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA
(NUTA)

na

MESSRS. PURSHOTAM PREMJI & SONS—MOSHI

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkataba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA) na P. Premji & Sons—Moshi, uliletwa mbele ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (b) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa ukiwa na mabadiliko yaliyokubaliwa na pande zote mbili.

Kibali hiki kitaanzia siku ya kwanza ya mwezi Oktoba, 1971.

MKATABA WA HIARI

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

MESSRS. PURSHOTAM PREMJI & SONS—MOSHI

1. Makubaliano:

Sisi Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA), tujulikanao hapa kwa jina "Chama" na Messrs. Purshotam Premji & Sons tujulikanao kwa jina "Muajiri" tunathibitisha hapa kwa maandishi na kutia sahihi zetu, kuonyesha kuwa, kwa uhuru na hiari yetu wenyewe tumekubaliana juu ya mambo haya yafuatayo kuhusu hali za kazi na mishahara.

2. Utambuzi:

(a) Muajiri anakitambua na kuheshimu haki za Chama, kuwa ndiye sauti na mtezi peke yake wa wafanyakazi wote walio wanachama wa NUTA kwa mambo yote yanayohusu hali za kazi na mishahara.

(b) Chama, kwa upande mwingine kinatambua Tajiri kuwa ndiye muajiri peke yake wa wafanyakazi wanaohusika na mkataba huu.

3. Kuhusika:

(a) Mkataba huu utawahusu wanachama wote wa Chama walio ajiriwa na Muajiri isipokuwa wale ambao ni wakuu wa kazi.

(b) Tafsiri ya Mkuu wa Kazi:

Tafsiri ya Mkuu wa Kazi itakuwa na maana ifuatayo:—

(i) Mkuu wa Kiwanda; au

(ii) Mkuu wa Kiwanda Msaidizi; au

(iii) Mkuu wa Idara; au

(iv) Mkurugenzi.

Vinginevyo, Mkuu wa kazi, ni mtu ye yote yule aliyepewa madaraka na uwezo kamili kwa maandishi wa kuajiri, kufukuza, na kuachisha kazi mfanyakazi, ama uwezo wa kupendekeza juu ya kuajiri, kumfukuza, na kumwachisha kazi mfanyakazi.

4. Muda na tarehe ya kuanza Mkataba:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba tarehe ya kuanza mkataba huu itakuwa 1 Oktoba, 1971 na utaendelea kutambuliwa kwa muda usiopungua miezi kumi na mbili (12). Katika muda huu, ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkataba huu, ni lazima afuate masharti yaliyomo katika fasili ya 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal), ya mwaka 1967.

(b) Hata hivyo mkataba unaweza kuvunjwa kwa makubaliano ya pande zote mbili, lakini ye yote katika hao anayetaka kuvunja kifungu cho chote inambidi atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa mwenzake kwa ajili ya kusudio hilo.

(c) Mkataba huu utaendelea kutambuliwa wakati wote mpaka wakati huo tu ambao labda mkataba utavunjwa, au kubadilishwa au kurekebisha kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

5. Kuajiri:

Muda wa majaribio utakuwa kama ifuatavyo:—

(a) Kwa kazi zinazohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya mwezi mmoja.

(b) Kwa kazi zinazohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya miezi miwili.

(c) Mara baada ya muda wa majaribio kumalizika mfanyakazi atahesabiwa kuwa ni mfanyakazi wa kudumu wa mwezi.

6. Uchaji au uachishwaji kazi:

(a) Katika muda wa majaribio upande wo wote:—

(i) Chini ya kifungu 5 (a) utatoa taarifa ya saa 24 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala ya taarifa hiyo.

(ii) Chini ya kifungu 5 (b) utatoa taarifa ya siku 14 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala yake.

(b) Kuhusu wafanyakazi wa kudumu, upande wo wote utatakiwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha ya mwezi mmoja badala ya taarifa hiyo. Taarifa hiyo, au malipo badala yake ni lazima itolewe kwa maandishi.

(c) Mfanyakazi asiachishwe kazi mpaka pamekuwapo na sababu ya maana inayoambatana na uwezo au tabia yake kazini au ustawi wa kazi.

Papo hapo yafuatayo yasiwe ni sababu ya kumwachisha kazi:—

(i) Kuwa mwanachama wa Chama au kufanya shughuli za Chama nje ya saa za kazi au wakati wa saa za kazi kwa idhini ya Tajiri au msimamizi wake wa kazi.

(ii) Kuwa mjumbe au kiongozi wa wafanyakazi au kugombea kiti cho chote cha ujumbe au uongozi wa wafanyakazi.

(iii) Kutoa malalamiko au kushiriki katika utaji wa ushahidi juu ya Tajiri kuvunja Sheria, kutokufuata siasa ya Taifa, au kufanya jambo lo lote la kuwaudhi wafanyakazi.

7. Nafasi za Kazi na Upunguzaji Wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kuwa, juhudi ya pamoja itafanya ili kuongeza nafasi za kazi na kuzuia upunguzaji wa wafanyakazi kazini, ili kusaidia Taifa katika kupambana na tatizo la ukosefu wa kazi za mishahara nchini.

(b) Hatua za kuwapunguza idadi ya wafanyakazi, zitachukuliwa tu, iwapo Tajiri atakitoshesha Chama, kuwa hakuna uwezekano wo wote mwingine wa kuepuka au kuzuia hatua hiyo. Hizi zifuatazo zitakuwa miongoni mwa njia zifaa zozote kufikiwa juu ya uepukaji wa upunguzaji wafanyakazi; uondaji wa kazi za ziada; ubadilishaji wa wafanyakazi kutoka sehemu wasikohitajiwa na kuwaweka kwenye sehemu nyingine ambazo zitaonekana kuwa na nafasi au haja na watu hao; kutoajiri tena, kwa muda, watu wapya mpaka hapo hali itakapordia tena kuwa njema; upunguzaji wa pole pole kwa wafanyakazi wote watakaohusika.

(c) Uchaguzi wa wafanyakazi watakaohusika na upunguzaji utafuata msingi wa "Wakwanza kuingia kazini awe wa mwisho kupunguzwa" au kufikiwa juu ya:—

(a) Haja ya utendaji bora wa kazi za kiwanda.

(b) Uwezo, uzoovu, ujuzi na sifa za kazi za kila mfanyakazi.

(c) Muda wa utumishi.

(d) Umri.

(e) Hali ya jamii yake.

(d) Wafanyakazi ambao wameachishwa kwa ajili ya upunguzaji lazima wapewe nafasi ya kwanza ya kurudishwa kazini wakati muajiri anapojiri wafanyakazi wapya. Kuajiriwa tena kufuate utaratibu uliotajwa hapo juu.

8. Saa za kazi:

(a) Saa za kazi zitakuwa 45 kwa juma. Jumapili na siku za Sikukuu kwa kawaida hakutakuwa na kazi.

(b) Kazi zote zitakazofanyika zaidi ya saa za kawaida, kwa juma au kwa mwezi zitaheesabika kuwa ni kazi ya ziada ambayo lazima italipwa kwa kiasi cha 1½ (moja na nusu) ya malipo ya saa za kawaida. Ila tu, ikiwa kazi hizo zitafanyika siku za Jumapili au Sikukuu za Kiserikali, basi malipo yake yatakuwa mara mbili ya kiasi cha malipo ya saa za kawaida.

9. Ulazima wa uanachama:

(a) Kila mfanyakazi aliyeajiriwa na Messrs. Purshotam Premji & Sons atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka tarehe ya mkataba huu kutangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali.

(b) Mfanyakazi ye yote yule mpya ambaye atakayeajiriwa baada ya mkataba huu kuanza kutumika atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi 2 mara baada ya kumaliza muda wake wa majaribio. Au ikiwa hatahusika na muda wa majaribio atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka amejiriwa.

(c) Mfanyakazi ye yote ambaye hatakuwa mwanachama wa Chama kwa mujibu wa Ibara hii atakuwa ametoa taarifa yake ya kuacha kazi.

10. Malipo ya kushikika kazi kwa muda:

Mfanyakazi anapohitajiwa na muajiri wake kushikika kwa muda kazi yenye madaraka na mshahara mkubwa zaidi kuliko wake ikiwa kupitana huku kwa mshahara ni kwa kiasi kisichopungua Sh. 100/- kwa mwezi, na iwapo atafanya kazi hiyo kwa muda wa zaidi ya wiki moja, italazimu Tajiri amlipe licha ya mshahara wake wa kawaida, sehemu yote ya mshahara wa kazi hiyo iliyozidi mshahara wake.

11. Nguo za kazi:

(a) Wafanyakazi wenye daraja hizi zifuatazo hapa chini wata-pewa jozi mbili za nguo kwa mwaka:—

1. Seremala.
2. Wasaidizi wa Seremala.

12. Ada za NUTA:

Imekubaliwa kwamba Muajiri atakuwa anakata ada za NUTA kila mwezi kutokana na mshahara wa kila mfanyakazi ambaye ni mwanachama wa NUTA na kuzituma pesa hizo kwenye Makao Makuu ya NUTA kupitia Mahesabu Na. 1 huko katika Tawi la Benki ya Taifa ya Biashara, Mtaa wa Market, Dar es Salaam.

13. Marupurupu:

Mambo yote yaliyotajwa hapa chini yatalipwa na Tajiri kwa mujibu wa "Sheria ya Marupurupu ya 1968":—

- (1) Likizo ya mwaka na malipo yake.
- (2) Likizo ya ugonjwa na malipo yake.
- (3) Likizo ya uzazi.
- (4) Likizo ya ugonjwa wa uzazi na malipo yake.
- (5) Likizo ya dharura.
- (6) Malipo ya safari ya likizo.

14. Mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba wafanyakazi wana-stahili kupewa mafunzo zaidi juu ya kazi zao ili waweze kutoa utumishi bora zaidi. Kwa ajili hiyo Tajiri ataweka mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi.

(b) Muajiri atatoa ruhusa bila ya kikwazo cho chote kwa mfanyakazi/wafanyakazi wakati wa saa za kazi wanapohitajiwa, ili kuhudhuria mafunzo ambayo mara kwa mara hutayarishwa na Chama, au Shirika lo lote la Taifa au vvyuo vinginevyo.

15. Matibabu:

(a) Matibabu yatatolewa bure kwa kila mfanyakazi pamoja na mkewe au mumewe na watoto wake.

(b) Kila mfanyakazi au jamaa yake anapohitaji kwenda kwenye matibabu Muajiri atampa cheti cha matibabu pamoja na chombo cha kusafiria kwenda huko.

16. Migogoro kazini:

(i) Migogoro yote itakayotokea kazini, kati ya Muajiri na mfanyakazi kazini ambayo inaweza kushughulikiwa chini ya Sheria ya Usalama Kazini, Na. 62 ya 1964 basi sheria hiyo itatumiwa kuondoa migogoro hiyo.

(ii) Migogoro au mabishano mengine ambayo hayaji chini ya Sheria Na. 62 ya Usalama Kazini ya mwaka 1964, usuluhishi wake utashughulikiwa kwanza kirafiki baina ya Kamati ya Kazi kama ipo, na Tajiri ili kufikia uelewano. Iwapo hatua hiyo haiatafauku mgogoro huo utapelekwa kwa Chama kwa kufuata ngazi zake. Kiwa bado usuluhishi haujapatikana, mgogoro huo utafuata Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi, 1967.

17. Mpango wa kukuza mazao:

Chama na Muajiri wamekubaliana kwamba watawafunza wafanyakazi wote juu ya haja na faida ya kukuza utumishi bora na mengine kazini, na kuweka mipango mbali mbali itakayoonekana kuwa itafaa ya kukuza utumishi bora.

18. Nyongeza ya mishahara:

(i) Imekubaliwa na pande zote mbili kwamba nyongeza za mishahara itakuwa kama hivi ifuatavyo:—

(ii) Wafanyakazi watatu (3) wapatao Sh. 185/- hadi Sh. 200/- watapata nyongeza ya Sh. 15/- kwa mwezi.

(iii) Wafanyakazi watatu (3) wapatao Sh. 260/- hadi Sh. 390/- watapata nyongeza ya Sh. 12/- kila mmoja kwa mwezi.

Mkataba huu umetiwa sahihi siku ya Jumatatu tarehe 4 Oktoba, 1971.

Kwa niaba ya

Messrs. P. Premji & Sons—Moshi

DEVJI PURSHOTAM
Partner Manager

Moshi,
18 Januari, 1972

Kwa niaba ya

Chama cha Taifa cha
Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

A. P. J. MWAKALINGA,
Katibu Msaidizi wa Tawi

SHABAN JUMA,
Mwakilishi wa Wafanyakazi

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 433

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Hiari Na. 217 wa 1971

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA
(NUTA)

na

M. O. KALYAN & SONS—ARUSHA

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkataba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA) na M. O. Kalyan & Sons uliletwa mbele ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (a) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa.

Kibali hiki kitaanzia siku ya kwanza ya mwezi Septemba, 1971.

MKATABA WA HIARI

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

M. O. KALYAN & SONS—ARUSHA

1. Makubaliano:

Sisi Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika, tujulikanao hapa kwa jina "Chama" na M. O. Kalyan & Sons tujulikanao kwa jina "Tajiri" tunathibitisha hapa kwa maandishi na kutia sahihi zetu, kuonyesha kuwa, kwa uhuru na hari yetu wenyewe tumekubaliana juu ya mambo haya yafuatayo kuhusu hali za kazi na mishahara.

2. Utambuzi:

(a) Tajiri anakitambua na kuheshimu haki za Chama, kuwa ndiye sauti na mtetezi peke yake wa wafanyakazi wote walio wanachama wa NUTA kwa mambo yote yanayohusu hali za kazi na mishahara.

(b) Chama, kwa upande mwingine kinatambua Tajiri kuwa ndiye Muajiri peke yake wa wafanyakazi wote wanaohusika na mkataba huu.

3. Kuhusika:

(a) Mkataba huu utawahusu wanachama wote wa Chama wali-ajiriwa na Tajiri isipokuwa wale ambao ni Wakuu wa kazi.

(b) Tafsiri ya Mkuu wa kazi:

Tafsiri ya Mkuu wa kazi itakuwa na maana ifuatayo:—

- (i) Mkuu wa Kiwanda; au
- (ii) Mkuu wa Kiwanda Msaidizi; au
- (iii) Mkuu wa Idara; au
- (iv) Mkurugenzi.

Vinginevyo, Mkuu wa kazi, ni mtu ye yote yule aliyepewa madaraka na uwezo kamili kwa maandishi wa kuajiri, kufukuza na kuachisha kazi mfanyakazi, ama uwezo wa kupendekeza juu ya kuajiri, kumfukuza, kumwachisha kazi mfanyakazi.

4. Muda na tarehe ya kuanza mkataba:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba tarehe ya kuanza mkataba huu itakuwa tarehe 1 Septemba, 1971 na utaendelea kutambuliwa kwa muda usiopugua miezi 12. Katika muda huu, ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkataba huu, ni lazima afuate masharti yaliyomo katika fasili ya 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal) ya mwaka 1967.

(b) Hata hivyo mkataba unaweza kuvunjwa kwa makubaliano ya pande zote mbili, lakini ye yote katika hao anayetaka kuvunja kifungu cho chote inambidi atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa mwenzake kwa ajili ya kusudio hilo.

(c) Mkataba huu utaendelea kutambuliwa wakati wote mpaka wakati huo tu ambao labda mkataba utavunjwa, au kubadilishwa au kurekebishwa kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

5. Kuajiri:

Muda wa majaribio utakuwa kama ifuatavyo:—

(a) Kwa kazi zisizohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya mwezi mmoja.

(b) Kwa kazi zinazohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya miezi miwili.

(c) Mara baada ya muda wa majaribio kumalizika mfanyakazi atahesabiwa kuwa ni mfanyakazi wa kudumu wa mwezi.

6. Uachaji au uachishwaji kazi:

(a) Katika muda wa majaribio upande wo wote:—

(i) Chini ya kifungu 5 (a) utatoa taarifa ya saa 24 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala ya taarifa hiyo.

(ii) Chini ya kifungu 5 (b) utatoa taarifa ya siku 14 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala yake.

(b) Kuhusu wafanyakazi wa kudumu, upande wote utatakiwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha ya mwezi mmoja badala ya taarifa hiyo. Taarifa hiyo, au malipo badala yake, ni lazima itolewe kwa maandishi.

(c) Mfanyakazi asiachishwe kazi mpaka pamekuwepo na sababu ya maana inayoambatana na uwezo au tabia yake kazini au ustawi wa kazi.

Papo hapo yafuatayo yasiwe ni sababu ya kumwachisha kazi:—

- (i) Kuwa mwanachama wa Chama au kufanya shughuli za Chama nje ya saa za kazi, au wakati wa saa za kazi kwa idhini ya Tajiri au msimamizi wake wa kazi.
- (ii) Kuwa mjumbe au kiongozi wa wafanyakazi au kugombea kiti cho chote cha ujumbe au uongozi wa wafanyakazi.
- (iii) Kutoa malalamiko au kushiriki katika utoaji wa ushahidi juu ya Tajiri kuvunja sheria, kutokufuata Siasa ya Taifa au kufanya jambo lo lote la kuwaudhi wafanyakazi.
- (iv) Ukabila, rangi, utu, dini, mawazo ya siasa na (Starche).

7. Nafasi za kazi na upunguzaji wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kuwa, juhudi ya pamoja itafanywa ili kuongeza nafasi za kazi na kuzuia upunguzwaji wa wafanyakazi kazini, ili kusaidia Taifa katika kupambana na tatizo la ukosefu wa kazi za mishahara nchini.

(b) Hatua za kuwapunguza idadi ya wafanyakazi, zitachukuliwa tu, iwapo Tajiri atakitosheliza Chama, kuwa, hakuna uwezekano wote mwingine wa kuepuka au kuzuia hatua hiyo. Hizi zifuatazo zitakuwa miongoni mwa njia zifaazo kufikiriwa juu ya uepukaji wa upunguzaji wafanyakazi; uondoaji wa kazi za ziada; ubadilishaji wa wafanyakazi kutoka sehemu wasiohitajiwa na kuwaweka kwenye sehemu nyingine ambazo zitaonekana kuwa na nafasi au haja na watu hao; kutoajiri tena, kwa muda watu wapya mpaka hapo hali itakaporudia tena kuwa njema; upunguzaji wa pole pole kwa wafanyakazi wote watakuhusika.

(c) Uchaguzi wa wafanyakazi watakuhusika na upunguzwaji utafuata msingi wa "Wakwanza kuingia kazini awe wa mwisho kupunguzwa" au kufikiriwa juu ya:—

- (a) Haja ya utendaji bora wa kazi za kiwanda.
- (b) Uwezo, uzoovu, ujuzi na sifa za kazi za kila mfanyakazi.
- (c) Muda wa utumishi.
- (d) Umri.
- (e) Hali ya jamii yake.
- (d) Wafanyakazi ambao wameachishwa kwa ajili ya upunguzaji lazima wapewe nafasi ya kwanza ya kurudishwa kazini wakati Muajiri anapojiri wafanyakazi wapya. Kuajiriwa tena kufuate utaratibu uliyotajwa hapo juu.

8. Saa za kazi:

(a) Saa za kazi zitakuwa 45 kwa juma. Jumapili na siku za Sikukuu kwa kawaida hakutakuwa na kazi.

(b) Kazi zote zitakazofanyika zaidi ya saa za kawaida kwa juma au kwa mwezi zitahesabika kuwa ni kazi ya ziada ambayo lazima italipwa kwa kiasi cha 1½ (moja na nusu) ya malipo ya saa za kawaida. Ila tu, ikiwa kazi hizo zitafanyika siku za Jumapili au Sikukuu za Kiserikali, basi malipo yake yatakuwa mara mbili ya kiasi cha malipo ya saa za kawaida.

9. Ulazima wa uanachama:

(a) Kila mfanyakazi aliyejiriwa na Tajiri atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa mezi miwili toka tarehe ya mkataba huu kutangazwa rasmi kwenye *Gazeti* la Serikali.

(b) Mfanyakazi ye yote yule mpya ambaye atakayejiriwa baada ya mkataba huu kuanza kutumika atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi 2 mara baada ya kumaliza muda wake wa majaribio. Au ikiwa hatahusika na muda wa majaribio atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka amejiriwa.

(c) Mfanyakazi ye yote ambaye hatakuwa mwanachama wa Chama kwa mujibu wa Ibara hii atakuwa ametoa taarifa yake ya kuacha kazi.

10. Malipo ya kushikika kazi kwa muda:

Mfanyakazi anapohitajiwa na Tajiri wake kushikika kwa muda kazi yenye madaraka na mishahara mkubwa zaidi kuliko wake na ikiwa kupitana huku kwa mishahara ni kwa kiasi kisichopungua Sh. 100/- kwa mwezi, na iwapo atafanya kazi hiyo kwa muda wa zaidi ya wiki moja, italazimu Tajiri amilipe licha ya mishahara wake wa kawaida, sehemu yote ya mishahara wa kazi hiyo iliyozidi mishahara wake.

11. Nguo za kazi:

(a) Wafanyakazi wenye daraja hizi zifuatazo hapa chini watapewa jozi mbili za nguo kwa mwaka:—

- (1) Tunboy.
- (2) Mtumishi wa ndani.

(b) Wafanyakazi wote ambao wamepewa nguo za kazi za kuhifadhi mwili itawalazimu kuzivaa katika nyakati zote za saa za kazi.

12. Ada za NUTA:

Imekubaliwa kwamba Tajiri atakuwa anakata ada za NUTA kila mwezi kutokana na mishahara wa kila mfanyakazi ambaye ni mwanachama wa NUTA na kuzituma pesa hizo kwenye Makao Makuu ya NUTA kupitia Mahesabu Na. 1 huko katika Tawi la Benki ya Taifa ya Biashara, Mtaa wa Market, Dar es Salaam.

13. Marupurupu:

Mambo yote yaliyotajwa hapa chini yatalipwa na Tajiri kwa mujibu wa "Sheria ya Marupurupu ya 1968":—

- (1) Likizo ya mwaka na malipo yake.
- (2) Likizo ya ugonjwa na malipo yake.
- (3) Likizo ya uzazi.
- (4) Likizo ya ugonjwa wa uzazi na malipo yake.
- (5) Likizo ya dharura.
- (6) Malipo ya safari ya likizo.

14. Mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba wafanyakazi wana-stahili kupewa mafunzo zaidi juu ya kazi zao ili waweze kutoa utumishi bora zaidi. Kwa ajili hiyo Tajiri ataweka mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi.

(b) Tajiri atatoa ruhusa bila kikwazo cho chote kwa mfanyakazi/wafanyakazi wakati wa saa za kazi wanapohitajiwa ili kuhudhuria mafunzo ambayo mara kwa mara hutayarishwa na Chama au Shirika lo lote la Taifa au vyo vinginevyo.

15. Matibabu:

(a) Matibabu yatatolewa bure kwa kila mfanyakazi pamoja na mkewe au mmewe na watoto wake.

(b) Kila mfanyakazi au jamaa yake anapohitaji kwenda kwenye matibabu Tajiri atampa cheti cha matibabu pamoja na chombo cha kusafiria kwenda huko.

16. Migogoro kazini:

(i) Migogoro yote itakayotokea kazini, kati ya Tajiri na mfanyakazi kazini ambayo inaweza kushughulikiwa chini ya Sheria ya Usalama Kazini Na. 62 ya 1964, basi Sheria hiyo itatumiwa kuondoa migogoro hiyo.

(ii) Migogoro au mabishano mengine ambayo hayaji chini ya Sheria Na. 62 ya Usalama Kazini ya mwaka 1964, usuluhishi wake utashughulikiwa kwanza kirafiki, baina ya Kamati ya Kazi kama ipo, na Tajiri ili kufikia uelewano. Iwapo hatua hiyo haifaulu mgogoro huo utapelekwa kwa Chama kwa kufuata ngazi zake. Ikiwa bado usuluhishi haujapatikana, mgogoro huo utafuata Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi, 1967.

17. Mpango wa kukuza mazao:

Chama na Tajiri wamekubaliana kwamba watawafunza wafanyakazi wote juu ya haja na faida ya kukuza utumishi bora na mengine kazini, na kuweka mipango mbali mbali itakayoonekana kuwa itafaa ya kukuza utumishi bora.

18. Nyongeza ya mishahara:

Imekubaliwa kwamba:—

Wafanyakazi 2 wanaopata Sh. 150/-—Sh. 165/- nyongeza itakuwa Sh. 13/- kwa mwezi kila mmoja.

Mfanyakazi 1 apataye mishahara zaidi ya Sh. 166/- nyongeza itakuwa Sh. 7/- kwa mwezi.

Kwa niaba ya

M. O. Kalyan & Sons

Chama cha Taifa cha
Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

H. G. CHIFUPA,
Katibu wa Tawi

L. W. NGANJI,
Katibu Msaidizi wa Tawi

SALIM RAJABU,
Mjumbe wa wafanyakazi

Moshi,
19 Januari, 1972

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 434

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Hiari Na. 218 wa 1971

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA
(NUTA)

na

NEW MWANANCHI RESTAURANT BOARDING &
LODGING, ARUSHA

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3. mkataba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA) na New Mwananchi Restaurant Boarding & Lodging, Arusha uliletwa mbele ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (b) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa ukiwa na mabadiliko yaliyokubaliwa na pande zote mbili.

Kibali hiki kitaanzia siku ya kwanza ya mwezi Septemba, 1971.

MKATABA WA HIARI

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

NEW MWANANCHI RESTAURANT BOARDING & LODGING, ARUSHA

1. Makubaliano:

Sisi Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika, tujulikanao hapa kwa jina "Chama" na New Mwananchi Restaurant Boarding & Lodging, tujulikanao kwa jina "Tajiri" tunathibitisha hapa kwa maandishi na kutia sahihi zetu kuonyesha kuwa, kwa uhuru na hiari yetu wenyewe tumekubaliana juu ya mambo haya yafuatayo kuhusu hali za kazi na mishahara.

2. Utambuzi:

(a) Tajiri anakitambua na kuheshimu haki za Chama, kuwa ndiye sauti na mtetezi peke yake wa wafanyakazi wote walio wanachama wa NUTA kwa mambo yote yanayohusu hali za kazi na mishahara.

(b) Chama, kwa upande mwingine kinatambua Tajiri kuwa ndiye Muajiri peke yake wa wafanyakazi wanaohusika na mkataba huu.

3. Kuhusika:

(a) Mkataba huu utawahusu wanachama wote wa Chama walio-ajiriwa na Tajiri isipokuwa wale ambao ni Wakuu wa kazi.

(b) *Tafsiri ya Mkuu wa kazi:*

Tafsiri ya Mkuu wa kazi itakuwa na maana ifuatayo:—

- (i) Mkuu wa Kiwanda; au
- (ii) Mkuu wa Kiwanda Msaidizi; au
- (iii) Mkuu wa Idara; au
- (iv) Mkurugenzi.

Vinginevyo, Mkuu wa kazi, ni mtu ye yote yule aliyepewa madaraka na uwezo kamili kwa maandishi ya kuajiri, kufukuza na kuachisha kazi mfanyakazi, ama uwezo wa kupendekeza juu ya kuajiri, kumfukuza na kumwachisha kazi mfanyakazi.

4. *Muda na tarehe ya kuanza mkataba:*

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba tarehe ya kuanza mkataba huu itakuwa tarehe 1 Septemba, 1971 na kuendelea kutambuliwa kwa muda usiopungua miezi kumi na mbili (12). Katika muda huu, ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkataba huu, ni lazima afuate masharti yaliyomo katika fasili ya 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal) ya mwaka 1967.

(b) Hata hivyo mkataba unaweza kuvunjwa kwa makubaliano ya pande zote mbili, lakini ye yote katika hao anayetaka kuvunja kifungu cho chote inambidi atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa mwenzake kwa ajili ya kusudio hilo.

(c) Mkataba huu utaendelea kutambuliwa wakati wote mpaka wakati huo tu ambao labda mkataba utavunjwa, au kubadilishwa au kurekebisha kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

5. *Kuajiri:*

Muda wa majaribio utakuwa kama ifuatavyo:—

(a) Kwa kazi zisizohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya mwezi mmoja.

(b) Kwa kazi zinazohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya miezi miwili.

(c) Mara baada ya muda wa majaribio kumalizika mfanyakazi atahesabiwa kuwa ni mfanyakazi wa kudumu wa mwezi.

6. *Uachaji au uachishwaji kazi:*

(a) Katika muda wa majaribio upande wo wote:—

(i) Chini ya kifungu 5 (a) utatoa taarifa ya saa 24 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala ya taarifa hiyo.

(ii) Chini ya kifungu 5 (b) utatoa taarifa ya siku 14 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala yake.

(b) Kuhusu wafanyakazi wa kudumu, upande wo wote utatakiwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha ya mwezi mmoja badala ya taarifa hiyo. Taarifa hiyo, au malipo badala yake, ni lazima itolewe kwa maandishi.

(c) Mfanyakazi asiachishwe kazi mpaka pamekuwepo na sababu ya maana inayoambatana na uwezo au tabia yake kazini au ustawi wa kazi.

Papo hapo yafuatayo yasiwe ni sababu ya kumwachisha kazi:—

(i) Kuwa mwanachama wa Chama au kufanya shughuli za Chama nje ya saa za kazi, au wakati wa saa za kazi kwa idhini ya Tajiri au msimamizi wake wa kazi.

(ii) Kuwa mjumbe au kiongozi wa wafanyakazi au kugombea kiti cho chote cha ujumbe au uongozi wa wafanyakazi.

(iii) Kutoa malalamiko au kushiriki katika utoaji wa ushahidi juu ya Tajiri kuvunja sheria, kutokufuata Siasa ya Taifa au kufanya jambo lo lote la kuwaudhi wafanyakazi.

(iv) Ukabila, rangi, utu, dini, mawazo ya siasa na (Starehe).

7. *Nafasi za kazi na upunguzaji wafanyakazi:*

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kuwa, juhudi ya pamoja itafanywa ili kuongeza nafasi za kazi na kuzuia upunguzwaji wa wafanyakazi kazini, ili kusaidia Taifa katika kupambana na tatizo la ukosefu wa kazi za mishahara nchini.

(b) Hatua za kuwapunguza idadi ya wafanyakazi, zitachukuliwa tu, iwapo Tajiri atakitoshleza Chama, kuwa, hakuna uwezekano wo wote mwingine wa kuepuka au kuzuia hatua hiyo. Hizi zifuatazo zitakuwa miongoni mwa njia zifaazo kufikiwa juu ya uepukaji wa upunguzaji wafanyakazi; uondoaji wa kazi za ziada; ubadilishaji wa wafanyakazi kutoka sehemu wasikohitajika na kuwaweka kwenye sehemu nyingine ambazo zitonekana kuwa na nafasi au haja na watu hao; kutoajiri tena, kwa muda watu wavya mpaka hapo hali itakaporudia tena kuwa njema; upunguzaji wa pole pole kwa wafanyakazi wote watakoahusika.

(c) Uchaguzi wa wafanyakazi watakoahusika na upunguzwaji utafuata msingi wa "Wakwanza kuingia kazini awe wa mwisho kupunguzwa" au kufikiwa juu ya:—

- (a) Haja ya utendaji bora wa kazi za kiwanda.
- (b) Uwezo, uzoovu, ujuzi na sifa za kazi za kila mfanyakazi.
- (c) Muda wa utumishi.
- (d) Umri.
- (e) Hali ya jamii yake.

(d) Wafanyakazi ambao wameachishwa kwa ajili ya upunguzaji lazima wapewe nafasi ya kwanza ya kurudishwa kazini wakati Muajiri anapojiri wafanyakazi wavya. Kuajiriwa tena kufuate utaratibu uliotajwa hapo juu.

8. *Saa za kazi:*

(a) Saa za kazi zitakuwa 48 kwa juma. Jumapili na siku za Sikukuu kwa kawaida hakutakuwa na kazi.

(b) Kazi zo zote zitakazofanyika zaidi ya saa za kawaida kwa juma au kwa mwezi zitahesabiwa kuwa ni kazi za ziada ambayo lazima italipwa kwa kiasi cha 1½ (moja na nusu) ya malipo ya saa za kawaida. Ila tu, ikiwa kazi hizo zitafanyika siku za Jumapili au Sikukuu za Kiserikali, basi malipo yake yatakuwa mara mbili ya kiasi cha malipo ya saa za kawaida.

9. *Ulazima wa uanachama:*

(a) Kila mfanyakazi aliyejiriwa na Tajiri atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka tarehe ya mkataba huu kutangazwa rasmi kwenye *Gazeti la Serikali*.

(b) Mfanyakazi ye yote yule mpya ambaye atakayejiriwa baada ya mkataba huu kuanza kutumika atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi 2 mara baada ya kumaliza muda wake wa majaribio. Au ikiwa hatahusika na muda wa majaribio atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka amejiriwa.

(c) Mfanyakazi ye yote ambaye hatakuwa mwanachama wa Chama kwa mujibu wa Ibara hii atakuwa ametoa taarifa yake ya kuacha kazi.

10. *Malipo ya kushikia kazi kwa muda:*

Mfanyakazi anapohitajiwa na Tajiri wake kushikia kwa muda kazi yenye madaraka na mshahara mkubwa zaidi kufiko wake na ikiwa kupitana huku kwa mshahara ni kwa kiasi kisichopungua Sh. 100/- kwa mwezi, na iwapo atafanya kazi hiyo kwa muda wa zaidi ya wiki moja, italazimu Tajiri amlipe licha ya mshahara wake wa kawaida, sehemu yote ya mshahara wa kazi hiyo iliyoziidi mshahara wake.

11. *Nguo za kazi:*

(a) Wafanyakazi wenye daraja hizi zifuatazo hapa chini wata-pewa jozi mbili za nguo kwa mwaka:—

- (1) Wafanyakazi wote wa Bar;
- (2) Wafanyakazi wote wa Hoteli.

(b) Wafanyakazi wote ambao wamepewa nguo za kazi za kuhifadhi mwili itawalazimu kuzivaa katika nyakati zote za saa za kazi.

12. *Ada za NUTA:*

Imekubaliwa kwamba Tajiri atakuwa anakata ada za NUTA kila mwezi kutokana na mshahara wa kila mfanyakazi ambaye ni mwanachama wa NUTA na kuzituma pesa hizo kwenye Makao Makuu ya NUTA kupitia Mahesabu Na. 1 huko katika Tawi la Benki ya Taifa ya Biashara, Mtaa wa Market, Dar es Salaam.

13. *Marupurupu:*

Mambo yote yaliyotajwa hapa chini yatalipwa na Tajiri kwa mujibu wa "Sheria ya Marupurupu ya 1968":—

- (1) Likizo ya mwaka na malipo yake.
- (2) Likizo ya ugonjwa na malipo yake.
- (3) Likizo ya uzazi.
- (4) Likizo ya ugonjwa wa uzazi na malipo yake.
- (5) Likizo ya dharura.
- (6) Malipo ya safari ya likizo.

14. *Mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi:*

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba wafanyakazi wana-stahili kupewa mafunzo zaidi juu ya kazi zao ili waweze kutoa utumishi bora zaidi. Kwa ajili hiyo Tajiri ataweka mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi.

(b) Tajiri atatoa ruhusa bila ya kikwazo cho chote kwa mfanyakazi/wafanyakazi wakati wa saa za kazi wanapohitajiwa, ili kuhudhuria mafunzo ambayo mara kwa mara hutayarishwa na Chama, au Shirika lo lote la Taifa au vyuo vinginevyo.

15. *Matibabu:*

(a) Matibabu yatatolewa bure kwa kila mfanyakazi pamoja na mkewe au mmewe na watoto wake.

(b) Kila mfanyakazi au jamaa yake anapohitaji kwenda kwenye matibabu Tajiri atampa cheti cha matibabu pamoja na chombo cha kusafirika kwenda huko.

16. *Migogoro kazini:*

(i) Migogoro yote itakayotokea kazini, kati ya Tajiri na mfanyakazi kazini ambayo inaweza kushughulikiwa chini ya Sheria ya Usalama Kazini Na. 62 ya 1964, basi Sheria hiyo itatumiwa kuondoa migogoro hiyo.

(ii) Migogoro au mabishano mengine ambayo hayaji chini ya Sheria Na. 62 ya Usalama Kazini ya mwaka 1964, usuluhishi wake utashughulikiwa kwanza kirafiki, baina ya Kamati ya Kazi kama ipo, na Tajiri ili kufikia uelewano. Iwapo hatua hiyo haitafaulu mgogoro huo utapelekwa kwa Chama kwa kufuata ngazi zake. Ikiwa bado usuluhishi haujapatikana, mgogoro huo utafuata Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi, 1967.

17. *Mpango wa kukuza mazao:*

Chama na Tajiri wamekubaliana kwamba watawafunza wafanyakazi wote juu ya haja na faida ya kukuza utumishi bora na mengine kazini, na kuweka mipango mbali mbali itakayoonekana kuwa itafaa ya kukuza utumishi bora.

18. *Nyongeza za mishahara:*

Imekubaliwa kwamba nyongeza itakuwa Sh. 13/- kwa kila mfanyakazi.

Kwa niaba ya
New Mwananchi Restaurant Boarding
& Lodging (Mto-wa-Mbu)

Kwa niaba ya
Chama cha Taifa cha
Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

H. G. CHIFUPA,
Katibu wa Tawi

L. W. NGANJI,
Katibu Msaidizi wa Tawi

Moshi,
19 Januari, 1972

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 435

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Hiari Na. 220 wa 1971

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

MESSRS. RONGAI UNITED TRANSPORT SERVICES LTD.

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkataba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA) na Messrs. Rongai United Transport Services Limited, uliletwa mbele ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (a) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa.

Kibali hiki kitaanzia siku ya kwanza ya mwezi Agosti, 1971.

MKATABA WA HIARI

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

MESSRS. RONGAI UNITED TRANSPORT SERVICES LIMITED

1. Makubaliano:

Sisi Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika, tujulikanao hapa kwa jina "Chama" na Messrs. Rongai United Transport Services Ltd. tujulikanao kwa jina "Muajiri" tunathibitisha hapa kwa maandishi na kutia sahihi zetu, kuonyesha kuwa, kwa uhuru na hiari yetu wenyewe tumekubaliana juu ya mambo haya yafuatayo kuhusu hali za kazi na mishahara.

2. Utambuzi:

(a) Muajiri anakitambua na kuheshimu haki za Chama, kuwa ndiye sauti na mtetezi peke yake wa wafanyakazi wote walio wanachama wa NUTA kwa mambo yote yanayohusu hali za kazi na mishahara.

(b) Chama, kwa upande mwingine kinatambua Tajiri kuwa ndiye muajiri peke yake wa wafanyakazi wanaohusika na mkataba huu.

3. Kuhusika:

(a) Mkataba huu utawahusu wanachama wote wa Chama walioajiriwa na Muajiri isipokuwa wale ambao ni Wakuu wa kazi.

(b) Tafsiri ya Mkuu wa Kazi:

Tafsiri ya Mkuu wa Kazi itakuwa na maana ifuatayo:—

- (i) Mkuu wa Kiwanda; au
- (ii) Mkuu wa Kiwanda Msaidizi; au
- (iii) Mkuu wa Idara; au
- (iv) Mkurugenzi.

Vinginevyo, Mkuu wa kazi, ni mtu ye yote yule aliyepewa madaraka na uwezo kamili kwa maandishi wa kuajiri, kufukuza, na kuachisha kazi mfanyakazi, ama uwezo wa kupendekeza juu ya kuajiri, kumfukuza, kumwachisha kazi mfanyakazi.

4. Muda na tarehe ya kuanza mkataba:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba tarehe ya kuanza mkataba huu itakuwa 1 Agosti, 1971 na utaendelea kutambuliwa kwa muda usiopungua miezi kumi na miwili. Katika muda huu, ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkataba huu, ni lazima afuate masharti yaliyomo katika fasili ya 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal) ya mwaka 1967.

(b) Hata hivyo mkataba unaweza kuvunjwa kwa makubaliano ya pande zote mbili lakini ye yote katika hao anayetaka kuvunja kifungu cho chote inambidi atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa mwenzake kwa ajili ya kusudio hilo.

(c) Mkataba huu utaendelea kutambuliwa wakati wote mpaka wakati huo tu, ambao labda mkataba utavunjwa, au kubadilishwa au kurekebishwa kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

5. Kuajiri:

Muda wa majaribio utakuwa kama ifuatavyo:—

(a) Kwa kazi zisizohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya mwezi mmoja.

(b) Kwa kazi zinazohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya miezi miwili.

(c) Mara baada ya muda wa majaribio kumalizika mfanyakazi atahesabiwa kuwa ni mfanyakazi wa kudumu wa mwezi.

6. Uchaji au uachishwaji kazi:

(a) Katika muda wa majaribio upande wo wote:—

(i) Chini ya kifungu 5 (a) utatoa taarifa ya saa 24 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala ya taarifa hiyo.

(ii) Chini ya kifungu 5 (b) utatoa taarifa ya siku 14 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala yake.

(b) Kuhusu wafanyakazi wa kudumu, upande wo wote utatakiwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha ya mwezi mmoja badala ya taarifa hiyo. Taarifa hiyo, au malipo badala yake, ni lazima itolewe kwa maandishi.

(c) Mfanyakazi asiachishwe kazi mpaka pamekuwepo na sababu ya maana inayoambatana na uwezo au tabia yake kazini au ustawi wa kazi.

Papo hapo yafuatayo yasiwe ni sababu ya kumwachisha kazi:—

- (i) Kuwa mwanachama wa Chama au kufanya shughuli za Chama nje ya saa za kazi, au wakati wa saa za kazi kwa idhini ya Tajiri au msimamizi wake wa kazi.

(ii) Kuwa mjumbe au kiongozi wa wafanyakazi au kugombea kiti cho chote cha ujumbe au uongozi wa wafanyakazi.

(iii) Kutoa malalamiko au kushiriki katika utoaji wa ushahidi juu ya Tajiri kuvunja sheria, kutofuata siasa ya Taifa au kufanya jambo lo lote la kuwaudhi wafanyakazi.

(iv) Ukabila, rangi, utu, dini, mawazo ya siasa na (Starehe).

7. Nafasi za kazi na upunguzaji wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kuwa, juhudi ya pamoja itafanywa ili kuongeza nafasi za kazi na kuzuia upunguzwaji wa wafanyakazi kazini, ili kusaidia Taifa katika kupambana na tatizo la ukosefu wa kazi za mishahara nchini.

(b) Hatua za kuwapunguza idadi ya wafanyakazi, zitachukuliwa tu, iwapo Tajiri atakitoshleza Chama, kuwa, hakuna uwezekano wo wote mwingine wa kuepuka au kuzuia hatua hiyo. Hizi zifuatazo zitakuwa miongoni mwa njia zifaazo kufikiriwa juu ya uepukaji wa upunguzaji wa wafanyakazi; uondoaji wa kazi za ziada; ubadilishaji wa wafanyakazi kutoka kwenye sehemu wasikohitajika na kuwaweka kwenye sehemu nyingine ambazo zitaonekana kuwa na nafasi au haja ya watu hao; kutoajiri tena, kwa muda, watu wapa mpaka hapo hali itakaporudia tena kuwa njema; upunguzaji wa pole pole kwa wafanyakazi wote watakoahusika.

(c) Uchaguzi wa wafanyakazi watakoahusika na upunguzwaji utafuata msingi wa "Wakwanza kuingia kazini awe wa mwisho kupunguzwa" au kufikiriwa juu ya:—

- (a) Haja ya utendaji bora wa kazi za kiwanda.
- (b) Uwezo, uzoovu, ujuzi na sifa za kazi za kila mfanyakazi.
- (c) Muda wa utumishi.
- (d) Umri.
- (e) Hali ya jamii yake.

(d) Wafanyakazi ambao wameachishwa kwa ajili ya upunguzaji lazima wapewe nafasi ya kwanza ya kurudishwa kazini wakati muajiri anapojiri wafanyakazi wapa. Kuajiriwa tena kutafuata utaratibu uliotajwa hapo juu.

8. Saa za kazi:

(a) Saa za kazi zitakuwa 45 kwa juma. Jumapili na siku za Sikukuu kwa kawaida hakutakuwa na kazi.

(b) Kazi zo zote zitakazofanyika zaidi ya saa za kawaida, kwa juma au kwa mwezi zitahesabiwa kuwa ni kazi za ziada ambayo lazima italipwa kwa kiasi cha 1½ (moja na nusu) ya malipo ya saa za kawaida. Ila tu, ikiwa kazi hizo zitafanyika siku za Jumapili au sikukuu za Kiserikali, basi malipo yake yatakuwa mara mbili ya kiasi cha malipo ya saa za kawaida.

9. Ulazima wa uanachama:

(a) Kila Mfanyakazi aliyejiriwa na Messrs. Rongai United Transport Services Ltd. atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka tarehe ya mkataba huu kutangazwa rasmi kwenye *Gazeti la Serikali*.

(b) Mfanyakazi ye yote yule mpya ambaye atakayejiriwa baada ya mkataba huu kuanza kutumika atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi 2 mara baada ya kumaliza muda wake wa majaribio. Au ikiwa hatahusika na muda wa majaribio atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka amejiriwa.

(c) Mfanyakazi ye yote ambaye hatakuwa mwanachama wa chama kwa mujibu wa Ibara hii atakuwa ametoa taarifa yake ya kuacha kazi.

10. Malipo ya kushikia kazi kwa muda:

Mfanyakazi anapohitajiwa na Muajiri wake kushikia kwa muda kazi yenye madaraka na mishahara mkubwa zaidi kuliko wake na ikiwa kupitana huku kwa mishahara ni kwa kiasi kisichopungua Sh. 100/- kwa mwezi, na iwapo atafanya kazi hiyo kwa muda wa zaidi ya wiki moja, italazimu Tajiri amilipe licha ya mishahara wake wa kawaida, sehemu yote ya mishahara wa kazi hiyo iliyozidi mishahara wake.

11. Ngao za kazi:

(a) Wafanyakazi wenye daraja hizi zifuatazo hapa chini watapewa jozi mbili za ngao kwa mwaka:—

- (1) Madreva.
- (2) Makondakta.
- (3) Mataniboi.
- (4) Makanika.

(b) Wafanyakazi wote ambao wampewa ngao za kazi za kuhifadhi mwili itawalazimu kuzivaa katika nyakati zote za saa za kazi.

12. Ada za NUTA:

Imekubaliwa kwamba Muajiri atakuwa anakata ada za NUTA kila mwezi kutokana na mishahara wa kila mfanyakazi ambaye ni mwanachama wa NUTA na kuzituma pesa hizo kwenye Makao Makuu ya NUTA kupitia Mahesabu Na. 1 huko katika Tawi la Benki ya Taifa ya Biashara, Mtaa wa Market, Dar es Salaam.

13. Marupurupu:

Mambo yote yaliyotajwa hapa chini yatalipwa na Tajiri kwa mujibu wa "Sheria ya Marupurupu ya 1968":—

- (1) Likizo ya mwaka na malipo yake.
- (2) Likizo ya ugonjwa na malipo yake.
- (3) Likizo ya uzazi.
- (4) Likizo ya ugonjwa wa uzazi na malipo yake.
- (5) Likizo ya dharura.
- (6) Malipo ya safari ya likizo.

14. Mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba wafanyakazi wana-stabili kupewa mafunzo zaidi juu ya kazi yao ili waweze kutoa utumishi bora zaidi. Kwa ajili hiyo Tajiri ataweka mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi.

(b) Muajiri atatoa ruhusa bila ya kikwazo cho chote kwa mfanyakazi/wafanyakazi wakati wa saa za kazi wanapohitajiwa, ili kuhudhuria mafunzo ambayo mara kwa mara hutayarishwa na Chama, au Shirika lo lote la Taifa au vyuo vinginevyo.

15. Matibabu:

(a) Matibabu yatatolewa bure kwa kila mfanyakazi pamoja na mkewe au mmmewe na watoto wake.

(b) Kila mfanyakazi au jamaa yake anapohitaji kwenda kwenye matibabu Tajiri atampa cheti cha matibabu pamoja na chombo cha kusafiria kwenda huko.

16. Migogoro kazini:

(i) Migogoro yote itakayotokea kazini, kati ya Muajiri na mfanyakazi kazini ambayo inaweza kushughulikiwa chini ya Sheria ya Usalama Kazini, Na. 62 ya 1964, basi sheria hiyo itatumiwa kuondoa migogoro hiyo.

(ii) Migogoro au mabishano mengine ambayo hayaji chini ya Sheria Na. 62 ya Usalama Kazini ya mwaka 1964 usuluhishi wake utashughulikiwa kwanza kirafiki, baina ya Kamati ya Kazi, kama ipo, na Tajiri ili kufikia uelewano. Iwapo hatua hiyo haifaulu migogoro huo utapelekwa kwa Chama kwa kufuata ngazi zake. Ikiwa bado usuluhishi haujapatikana, mgogoro huo utafuata Sheria ya Baraza la Kudumu la Wafanyakazi, 1967.

17. Mpango wa kukuza mazao:

Chama na Muajiri wamekubaliana kwamba watawafunza wafanyakazi wote juu ya haja na faida ya kukuza utumishi bora na mengine kazini, na kuweka mipango mbali mbali itakayoonekana kuwa itafaa ya kukuza utumishi bora.

18. Nyongeza ya mshahara:

(a) Imekubaliwa na pande zote mbili kwamba nyongeza za mishahara itakuwa kama hivi ifuatavyo:—

(i) Wafanyakazi wanne (4) wapatao mshahara Sh. 120/- hadi Sh. 150/- wataongezwa Sh. 18/- kwa mwezi.

(ii) Wafanyakazi watatu (3) wapatao mshahara wa Sh. 300/- watapata nyongeza ya Sh. 13/- kwa mwezi.

(iii) Wafanyakazi 2 wapatao Sh. 350/- hadi Sh. 500/- watapata nyongeza ya Sh. 10/- kwa mwezi.

Mkatamba huu umetiwa sahihi siku ya Ijumaa tarehe 1 Oktoba, mwaka elfu moja mia tisa sabini na moja.

Kwa niaba ya

Messrs. *Rongai United Transport Services Limited*

F. S. MTENGA,
Mkurugenzi

Kwa niaba ya

Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika

A. P. J. MWAKALINGA,
Katibu Msaidizi
MAIKO JOSEPH,
Mjumbe wa Wafanyakazi

Moshi,

19 Januari, 1972

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 436

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkatamba wa Hiari Na. 223 wa 1971

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

TANZANIA WIRE PRODUCTS LIMITED, DAR ES SALAAM

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkatamba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA) na Tanzania Wire Products Limited, Dar es Salaam, uliletwa mbele ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (b) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkatamba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa ukiwa na mabadiliko yaliyokubaliwa na pande zote mbili.

Kibali hiki kitaanzia kutoka Septemba, 1971.

MKATABA WA HIARI

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

TANZANIA WIRE PRODUCTS LIMITED, DAR ES SALAAM

1. Makubaliano:

Sisi tujulikanao tukiwa wote wawakilishi wa pande zote mbili tumekubaliana hali za kazi na mambo ya mishahara ifuatayo hapa chini:—

2. Muda na tarehe ya kuanza mkatamba:

Mkatamba huu utanzia kutoka Septemba, 1971 na utaendelea kutambuliwa kwa muda wa miezi 24. Katika muda huo ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkatamba huu, atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa ajili ya kusudio hilo.

Pia ikiwa ni kufuta au kubadilisha kifungu cho chote cha mkatamba huu ni lazima ifuatwe masharti yaliyomo katika fasili 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal), 1967.

Hata hivyo mkatamba huu utaendelea kutambuliwa mpaka wakati huo tu ambao labda mkatamba utavunjwa au kubadilishwa au kurekebisha kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

3. Nyongeza:

Tumekubaliana sote kwamba nyongeza zitolewa kila baada ya mwaka mmoja kumaliza kama hivi ifuatavyo:—

(a) Wafanyakazi 13 wapatao toka Sh. 180/- hadi Sh. 200/- kwa mwezi watapata nyongeza ya Sh. 13/- kwa mwezi.

(b) Wafanyakazi 12 wapatao toka Sh. 201/- hadi Sh. 300/- kwa mwezi watapata nyongeza ya Sh. 10/- kwa mwezi.

(c) Wafanyakazi 2 wapatao toka Sh. 301/- na kuendelea kwa mwezi watapata Sh. 10/- kwa mwezi.

4. Hali nyingine za kazi:

Tumekubaliana ya kama hali za kazi zilizopo kwenye mkatamba wetu uliopita zitaendelea kutambulikana ila labda kuwepo na mabadiliko ya Sheria ya Marupurupu ya mwaka 1968.

Mkatamba huu umetiwa sahihi siku ya tarehe 22 Oktoba, 1971.

Kwa niaba ya

Tanzania Wire Products Limited

Kwa niaba ya

Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika

B. A. MFINANGA,
Katibu wa Mkoa

J. A. MHANDO,
Katibu wa Tawi

M. A. MAMBOYA,
Katibu Msaidizi wa Tawi

Mwenyekiti, Kamati ya Kazi

Dar es Salaam,

26 Januari, 1972

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 437

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkatamba wa Hiari Na. 231 wa 1971

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

H. H. THE AGA KHAN HOSPITAL—DAR ES SALAAM

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkatamba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA) na H. H. The Aga Khan Hospital—Dar es Salaam uliletwa mbele ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (b) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkatamba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa ukiwa na mabadiliko yaliyokubaliwa na pande zote mbili.

Kibali hiki kitaanzia siku ya kwanza Novemba, 1971.

MKATABA WA HIARI

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

H. H. THE AGA KHAN HOSPITAL—DAR ES SALAAM

1. Makubaliano:

Sisi tujulikanao tukiwa wote wawakilishi wa pande zote mbili tumekubaliana hali za kazi na mambo ya mishahara ifuatayo hapa chini.

2. Muda na tarehe ya kuanza mkatamba:

Mkatamba huu utanzia tarehe 1 Novemba, 1971 na utaendelea kutambuliwa kwa muda usiopungua miezi 24. Katika muda huo ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkatamba huu, atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa ajili ya kusudio hilo.

Pia ikiwa ni kufuta au kubadilisha kifungu cho chote cha mkatamba huu ni lazima ifuatwe masharti yaliyomo katika fasili 27 ya (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal) ya 1967.

Hata hivyo mkatamba huu utaendelea kutambuliwa mpaka wakati huo tu ambao labda mkatamba utavunjwa au kubadilishwa au kurekebisha kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

3. Nyongeza:

Tumekubaliana sote kwamba nyongeza hizi hizi zitolewa tena baada ya mwaka mmoja kumalizika kama hivi ifuatavyo:—

(a) Wafanyakazi 50 wapatao toka Sh. 199/- mpaka Sh. 250/- kwa mwezi watapata nyongeza ya Sh. 19/- kwa mwezi.

(b) Wafanyakazi 17 wapatao toka Sh. 251/- mpaka Sh. 350/- kwa mwezi watapata nyongeza ya Sh. 17/50 kwa mwezi.

(c) Wafanyakazi 28 wapatao toka Sh. 351/- na zaidi kwa mwezi watapata Sh. 20/30 kwa mwezi.

4. Hali nyingine za kazi:

Tumekubaliana ya kama hali za kazi zilizopo kwenye mkatamba wetu uliopita zitaendelea kutambulikana ila labda kuwepo na mabadiliko ya "Sheria ya Marupurupu ya mwaka 1968".

Mkatamba huu umetiwa sahihi siku ya Alhamisi tarehe 14 Oktoba, 1971.

Kwa niaba ya

H. H. Aga Khan Hospital

Kwa niaba ya
Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

Acting Chairman

B. A. MFINANGA,
Katibu wa Mkoa

J. A. MHANDO,
Katibu wa Tawi

M. S. MAMBOYA,
Katibu Msaidizi wa Tawi

S. KITOLA,
Mwenyekiti, Kamati ya Wafanyakazi

Dar es Salaam,

2 Februari, 1972

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 438

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Hiari Na. 240 wa 1971

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

BUKOLI BUS SERVICE, GEITA

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkataba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA na Bukoli Bus Service, Geita uliletwa mbele ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (a) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa.

Kibali hiki kitaanzia siku ya kwanza ya mwezi Oktoba, 1971.

MKATABA WA HIARI

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

BUKOLI BUS SERVICE, GEITA

1. Makubaliano:

Sisi Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika, tujulikanao hapa kwa jina "Chama" na Bukoli Bus Service, tujulikanao kwa jina "Tajiri" tunathibitisha hapa kwa maandishi na kuti sahihi zetu, kuonyesha kuwa, kwa uhuru na hiari yetu wenyewe tumekubaliana juu ya mambo haya yafuatayo kuhusu hali za kazi na mishahara.

2. Utambuzi:

(a) Tajiri anakitambua na kuheshimu haki za Chama, kuwa ndiye sauti na mtetezi peke yake wa wafanyakazi wote walio wanachama wa NUTA kwa mambo yote yanayohusu hali za kazi na mishahara.

(b) Chama, kwa upande mwingine kinatambua Tajiri kuwa ndiye muajiri peke yake wa wafanyakazi wanaohusika na mkataba huu.

3. Kuhusika:

(a) Mkataba huu utawahusu wanachama wote wa Chama walioajiriwa na Tajiri isipokuwa wale ambao ni Wakuu wa kazi.

(b) Tafsiri ya Mkuu wa kazi:

Tafsiri ya Mkuu wa kazi itakuwa na maana ifuatayo:—

- (i) Mkuu wa Kiwanda; au
- (ii) Mkuu wa Kiwanda Msaidizi; au
- (iii) Mkuu wa Idara; au
- (iv) Mkurugenzi.

Vinginevyo, Mkuu wa kazi, ni mtu ye yote yule aliyepewa madaraka na uwezo kamili kwa maandishi ya kuajiri, kufukuza, na kuachisha kazi mfanyakazi, ama uwezo wa kupendekeza juu ya kuajiri, kumfukuza, na kumwachisha kazi mfanyakazi.

4. Muda na tarehe ya kuanza mkataba:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba tarehe ya kuanza mkataba huu itakuwa tarehe 1 Oktoba, 1971 na utaendelea kutambuliwa kwa muda usiopungua miezi kumi na miwili. Katika muda huu, ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkataba huu, ni lazima afuate masharti yaliyomo katika fasili ya 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal) ya mwaka 1967.

(b) Hata hivyo mkataba unaweza kuvunjwa kwa makubaliano ya pande zote mbili, lakini ye yote katika hao anayetaka kuvunja kifungu cho chote inambidi atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa mwenzake kwa ajili ya kusudio hilo.

(c) Mkataba huu utaendelea kutambuliwa wakati wote mpaka wakati huo tu ambao labda mkataba utavunjwa, au kubadilishwa au kurekebishwa kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

5. Kuajiri:

Muda wa majaribio utakuwa kama ifuatavyo:—

(a) Kwa kazi zisizohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya mwezi mmoja.

(b) Kwa kazi zinazohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya miezi miwili.

(c) Mara baada ya muda wa majaribio kumalizika mfanyakazi atahesabiwa kuwa ni mfanyakazi wa kudumu wa mwezi.

6. Uchaji au uchishwaji kazi:

(a) Katika muda wa majaribio upande wote:—

(i) Chini ya kifungu 5 (a) utatoka taarifa ya saa 24 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala ya taarifa hiyo.

(ii) Chini ya kifungu 5 (b) utatoka taarifa ya siku 14 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala yake.

(b) Kuhusu wafanyakazi wa kudumu, upande wote utatakiwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha ya mwenzi mmoja badala ya taarifa hiyo. Taarifa hiyo, au malipo badala yake, ni lazima itolewe kwa maandishi.

(c) Mfanyakazi asiachishwe kazi mpaka pamekuwepo na sababu ya maana inayoambatana na uwezo au tabia yake kazini au ustawi wa kazi.

Papo hapo yafuatayo yasiwe ni sababu ya kumwachisha kazi:—

- (i) Kuwa mwanachama wa Chama au kufanya shughuli za Chama nje ya saa za kazi, au wakati wa saa za kazi kwa idhini ya Tajiri au msimamizi wake wa kazi.
- (ii) Kuwa mjumbe au kiongozi wa wafanyakazi au kugombea kiti cho chote cha ujumbe au uongozi wa wafanyakazi.

(iii) Kutoa majalamiko au kushiriki katika utoaji wa ushabidi juu ya Tajiri kuvunja sheria, kutokufuata siasa ya Taifa au kufanya jambo lo lote la kuwaudhi wafanyakazi.

(iv) Ukabila, rangi, utu, dini, mawazo ya siasa na (Starehe).

7. Nafasi za kazi na upunguzaji wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kuwa, juhudi ya pamoja itafanywa ili kuongeza nafasi za kazi na kuzuia upunguzwaji wa wafanyakazi kazini, ili kusaidia Taifa katika kupambana na tatizo la ukosefu wa kazi za mishahara nchini.

(b) Hatua za kuwapunguza idadi ya wafanyakazi, zitachukuliwa tu, iwapo Tajiri atakitoshesha Chama, kuwa, hakuna uwezekano wote mwingine wa kuepuka au kuzuia hatua hiyo. Hizi zifuatazo zitakuwa miongoni mwa njia zifaazo kufikiriwa juu ya uepukaji wa upunguzaji wafanyakazi; uondoaji wa kazi za ziada; ubadilishaji wa wafanyakazi kutoka sehemu wasikohitajiwa na kuwaweka kwenye sehemu nyingine ambazo zitaonekana kuwa na nafasi au haja na watu hao; kutoajiri tena, kwa muda, watu wapya mpaka hapo hali itakaporudia tena kuwa njema; upunguzaji wa pole pole kwa wafanyakazi wote watakaohusika.

(c) Uchaguzi wa wafanyakazi watakaohusika na upunguzwaji utafuata msingi wa "Wakwanza kuingia kazini awe wa mwisho kupunguzwa" au kufikiriwa juu ya:—

- (a) Haja ya utendaji bora wa kazi ya kiwanda.
- (b) Uwezo, uzoovu, ujuzi na sifa za kazi za kila mfanyakazi.
- (c) Muda wa utumishi.
- (d) Umri.
- (e) Hali ya jamii yake.

(d) Wafanyakazi ambao wameachishwa kwa ajili ya upunguzaji lazima wapewe nafasi ya kwanza ya kurudishwa kazini wakati Tajiri anapojiri wafanyakazi wapya. Kuajiriwa tena kutafuata utaratibu uliotajwa hapo juu.

8. Saa za kazi:

(a) Saa za kazi zitakuwa 48 kwa juma. Jumapili na siku za Sikukuu kwa kawaida hakutakuwa na kazi.

(b) Kazi zote zitakazofanyika zaidi ya saa za kawaida kwa juma au kwa mwezi zitahesabiwa kuwa ni kazi za ziada ambazo lazima zitalipwa kwa kiasi cha 1½ (moja na nusu) ya malipo ya saa za kawaida. Ila tu, ikiwa kazi hizo zitafanyika siku za Jumapili au Sikukuu za Kiserikali, basi malipo yake yatakuwa mara mbili ya kiasi cha malipo ya saa za kawaida.

9. Ulazima wa Uanachama:

(a) Kila mfanyakazi aliyejajiriwa na Bukoli Bus Service atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka tarehe ya mkataba huu kutangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali.

(b) Mfanyakazi ye yote yule mpya ambaye atakayejajiriwa baada ya mkataba huu kuanza kutumika atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi 2 mara baada ya kumaliza muda wake wa majaribio. Au ikiwa hatahusika na muda wa majaribio atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka amejajiriwa.

(c) Mfanyakazi ye yote ambaye hatakuwa mwanachama wa Chama kwa mujibu wa Ibara hii atakuwa ametoa taarifa yake ya kuacha kazi.

10. Malipo ya kushikia kazi kwa muda:

Mfanyakazi anapohitajiwa na Tajiri wake kushikia kwa muda kazi yenye madaraka na mishahara mkubwa zaidi kuliko wake na ikiwa kupitana huku kwa mishahara ni kwa kiasi kisichopungua Sh. 100/- kwa mwezi, na iwapo atafanya kazi hiyo kwa muda wa zaidi ya wki moja, italazimu Tajiri amilipe licha ya mishahara wake wa kawaida, sehemu yote ya mishahara wa kazi hiyo iliyozidi mishahara wake.

11. Nguo za kazi:

(a) Wafanyakazi wenye daraja hizi zifuatazo hapa chini watapewa jozi mbili za nguo kwa mwaka:—

- (1) Dreva.
- (2) Condakta.
- (3) Taniboi.

(b) Wafanyakazi wote ambao wamepelewa nguo za kuhifadhi miwili itawalazimu kuzivaa katika nyakati zote za saa za kazi.

12. Ada za NUTA:

Imekubliwa kwamba Tajiri atakuwa anakata ada za NUTA kila mwezi kutokana na mishahara wa kila mfanyakazi ambaye ni mwanachama wa NUTA na kuzituma pesa hizo katika Ofisi ya NUTA, Mwanza.

13. Marupurupu:

Mambo yote yaliyotajwa hapa chini yatalipwa na Tajiri kwa mujibu wa "Sheria ya Marupurupu ya 1968":—

- (1) Likizo ya mwaka na malipo yake.
- (2) Likizo ya uzazi.
- (3) Likizo ya ugonjwa na malipo yake.
- (4) Likizo ya ugonjwa wa uzazi na malipo yake.
- (5) Likizo ya dharura.
- (6) Malipo ya safari ya likizo.

14. Mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba wafanyakazi wana-stahili kupewa mafunzo zaidi juu ya kazi yao ili waweze kutoa utumishi bora zaidi. Kwa ajili hiyo Tajiri ataweka mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi.

(b) Tajiri atatoa ruhusa bila ya kikwazo cho chote kwa mfanyakazi/wafanyakazi wakati wa saa za kazi wanapohitajiwa, ili kuhudhuria mafunzo ambayo mara kwa mara hutayarishwa na Chama, au Shirika lo lote la Taifa au vyuo vinginevyo.

15. Matibabu:

Tajiri atatoa cheti kwa wafanyakazi ili waweze kupata matibabu katika Hospitali ya Serikali.

16. Migogoro kazini:

(i) Migogoro yote itakayotokea kazini, kati ya Tajiri na mfanyakazi kazini ambayo inaweza kushughulikiwa chini ya Sheria ya Usalama Kazini Na. 62 ya 1964 basi sheria hiyo itatumwa kuondoa migogoro hiyo.

(ii) Migogoro au mabishaio mengine ambayo hayaji chini ya Sheria Na. 62 ya Usalama Kazini ya mwaka 1964, usuluhishi wake utashughulikiwa kwanza Kiwandani, baina ya Kamati ya Kazi kama ipo, na Tajiri ili kufikia uelewano. Iwapo hatua hiyo haitafaulu mgogoro huo utapelekwa kwa Chama kwa kufuata ngazi zake. Ikiwa bado usuluhishi haujapatikana, mgogoro huo utafuata Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi, 1967.

17. Mpango wa kukuza mazao:

Chama na Tajiri wamekubaliana kwamba watawafunza wafanyakazi wote juu ya haja na faida ya kukuza utumishi bora na mengine kazini, na kuweka mipango mbali mbali itakayoonekana kuwa itafaa ya kukuza utumishi bora.

18. Posho ya safari:

Ikiwa mfanyakazi atasafiri kwa muda tu kwenda kazini mahali pengine mbali ya pale mahali pake pa kawaida anapofanyia kazi, atalipwa posho ya safari kama hivi ifuatavyo:—

Ikiwa safari na kazi hiyo ni kutoka asubuhi mpaka jioni posho itakuwa Sh. 7/- Dreva, Condakta Sh. 5/- na Taniboi Sh. 4/-.

19. Nyongeza za mishahara:

Imekubaliwa kwamba nyongeza ya mishahara itakuwa kama ifuatavyo:—

Wafanyakazi 4 wanaopata mishahara kuanzia Sh. 130/- mpaka Sh. 190/- wataongezwa Sh. 13/- kila mtu.

Wafanyakazi 2 wanaopata Sh. 191/- na zaidi wataongezwa Sh. 10/- kila mtu.

Mkataba huu umetiwa sahihi siku ya Jumanne tarehe 28 Septemba, 1971.

Kwa niaba ya
Bukoli Bus Service, Geita

Kwa niaba ya
Chama cha Taifa cha
Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

SAIDI MBARAK,
Meneja

M. K. J. MATOKE,
Katibu wa Mkoa

J. C. M. MANG'ONDI,
Katibu wa Tawi

Wajumbe wa Wafanyakazi

Dar es Salaam
26 Januari, 1972

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 439

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Hiari Na. 243 wa 1971

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

MESSRS. SIMU YA UPEPO BUS SERVICE—MWANZA

Kwa kufuata na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkataba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA) na Messrs. Simu ya Upepo Bus Service—Mwanza uliletwa mbele ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (a) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa.

Kibali hiki kitaanza siku ya kwanza ya mwezi wa Oktoba, 1971.

MKATABA WA HIARI

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

MESSRS. SIMU YA UPEPO BUS SERVICE—MWANZA

1. Makubaliano:

Sisi Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika, tujulikanao hapa kwa jina "Chama" na Smu ya Upepo Bus Service tujulikanao kwa jina "Tajiri" tunathibitisha hapa kwa maandishi na kutia sahihi zetu, kuonyesha kuwa kwa uhuru na hiari yetu wenyewe tumekubaliana juu ya mambo haya yafuatayo kuhusu hali za kazi na mishahara.

2. Utambuzi:

(a) Tajiri anakitambua na kuheshimu haki za Chama, kuwa ndicho sauti na mtezi peke yake wa wafanyakazi wote walio wanachama wa NUTA kwa mambo yote yanayohusu hali za kazi na mishahara.

(b) Chama, kwa upande mwingine kinatambua Tajiri kuwa ndiye muajiri peke yake wa wafanyakazi wanaohusika na mkataba huu.

3. Kuhusika:

(a) Mkataba huu utawahusu wanachama wote wa Chama walioajiriwa na Tajiri isipokuwa wale ambao ni wakuu wa kazi.

(b) Tafsiri ya Mkuu wa Kazi:

Tafsiri ya Mkuu wa Kazi itakuwa na maana ifuatayo:—

- (i) Mkuu wa Kiwanda; au
- (ii) Mkuu wa Kiwanda Msaidizi; au
- (iii) Mkuu wa Idara; au
- (iv) Mkurugenzi.

Vinginevyo, Mkuu wa Kazi, ni mtu ye yote yule aliyepewa madaraka na uwezo kamili kwa maandishi wa kuajiri, kufukuza, na kuachisha kazi mfanyakazi, ama uwezo wa kupendekeza juu ya kuajiri, kumfukuza na kumwachisha kazi mfanyakazi.

4. Muda na tarehe ya kuanza mkataba:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba tarehe ya kuanza mkataba huu itakuwa 1 Oktoba, 1971 na utaendelea kutambuliwa kwa muda usiopungua miezi 12. Katika muda huu, ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkataba huu, ni lazima afuate masharti yaliyomo katika fasili ya 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal) ya mwaka 1967.

(b) Hata hivyo mkataba unaweza kuvunjwa kwa makubaliano ya pande zote mbili, lakini ye yote katika hao anayetaka kuvunja kifungu cho chote inambidi atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa mwenzake kwa ajili ya kusudio hilo.

(c) Mkataba huu utaendelea kutambuliwa wakati wote mpaka wakati huo tu ambao labda mkataba utavunjwa, au kubadilishwa au kurekebisha kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

5. Kuajiri:

Muda wa majaribio utakuwa kama ifuatavyo:—

- (a) Kwa kazi zisizohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya mwezi mmoja.
- (b) Kwa kazi zinazohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya miezi miwili.
- (c) Mara baada ya muda wa majaribio kumalizika mfanyakazi atahesabiwa kuwa ni mfanyakazi wa kudumu wa mwezi.

6. Uchaji au Uachishwaji kazi:

(a) Katika muda wa majaribio upande wo wote:—

- (i) Chini ya kifungu 5 (a) utatoa taarifa ya saa 24 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala ya taarifa hiyo.
- (ii) Chini ya kifungu 5 (b) utatoa taarifa ya siku 14 ya taarifa ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala yake.

(b) Kuhusu wafanyakazi wa kudumu, upande wo wote utatakiwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha ya mwezi mmoja badala ya taarifa hiyo. Taarifa hiyo, au malipo badala yake, ni lazima itolewe kwa maandishi.

(c) Mfanyakazi asiachishwe kazi mpaka pamekuwapo na sababu ya maana inayoambatana na uwezo au tabia yake kazini au ustawi wa kazi.

Papo hapo yafuatayo yasiwe ni sababu ya kumwachisha kazi:—

- (i) Kuwa mwanachama wa Chama au kufanya shughuli za Chama nje ya saa za kazi, au wakati wa saa za kazi kwa idhini ya Tajiri au msimamizi wake wa kazi.
- (ii) Kuwa mjumbe au Kiongozi wa Wafanyakazi au kugombea kiti cho chote cha ujumbe au uongozi wa wafanyakazi.
- (iii) Kutoa malalamiko au kushiriki katika utoaji wa ushahidi juu ya Tajiri kuvunja sheria, kutokufuata siasa ya Taifa, au kufanya jambo lo lote la kuwaudhi wafanyakazi.
- (iv) Ukabila, rangi, utu, dini, mawazo ya siasa na (starehe).

7. Nafasi za kazi na Upunguzaji wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kuwa, juhudi ya pamoja itafanywa ili kuongeza nafasi za kazi na kuzuia upunguzaji wa wafanyakazi kazini, ili kusaidia Taifa katika kupambana na tatizo la ukosefu wa kazi za mishahara nchini.

(b) Hatua za kuwapunguza idadi ya wafanyakazi, zitachukuliwa tu, iwapo Tajiri atakitotosheleza Chama, kuwa, hakuna uwezekano wo wote mwingine wa kuepuka au kuzuia hatua hiyo. Hizi zifuatazo zitakuwa miongoni mwa njia zifaazo kufikiriwa juu ya uepukaji wa upunguzaji wa wafanyakazi; uondoaji wa kazi za ziada; ubadilishaji wa wafanyakazi kutoka sehemu wasiohitajika na kuwaweka kwenye sehemu nyingine ambazo zitaonekana kuwa na nafasi au haja na watu hao; kutoajiri tena kwa muda, watu wavya mpaka hapo hali itakaporudia tena kuwa njema; upunguzaji wa pole pole kwa wafanyakazi wote watakoahusika.

(c) Uchaguzi wa wafanyakazi utakoahusika na upunguzaji utafuata msingi wa "Wakwanza kuingia kazini awe wa mwisho kupunguzwa" au kufikiriwa juu ya:—

- (a) Haja ya utendaji bora wa kazi za kiwanda.
- (b) Uwezo, uzoovu, ujuzi na sifa za kazi za kila mfanyakazi.
- (c) Muda wa utumishi.
- (d) Umri.
- (e) Hali ya jamii yake.

(d) Wafanyakazi ambao wameachishwa kwa ajili ya upunguzaji lazima wapewe nafasi ya kwanza ya kurudishwa kazini wakati Tajiri anapojiri wafanyakazi wavya. Kuajiriwa tena kutafuta utaratibu uliyotajwa hapo juu.

8. Saa za kazi:

(a) Saa za kazi zitakuwa 48 kwa juma. Jumapili na Siku za Sikukuu kwa kawaida hakutakuwa na kazi.

(b) Kazi zo zote zitakazofanyika zaidi ya saa za kawaida, kwa juma au kwa mwezi zitahesabika kuwa ni kazi za ziada ambayo lazima italipwa kwa kiasi cha 1½ (moja na nusu) ya malipo ya saa za kawaida. Ila tu, ikiwa kazi hizo zitafanyika siku za Jumapili au Sikukuu za Kiserikali, basi malipo yake yatakuwa mara mbili ya kiasi cha malipo ya saa za kawaida.

9. Ulazima wa uanachama:

(a) Kila mfanyakazi aliyejajiriwa na Messrs. Simu ya Upepo Bus Service atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka tarehe ya mkataba huu kutangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali.

(b) Mfanyakazi ye yote yule mpya ambaye atakajiriwa baada ya mkataba huu kuanza kutumika atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi 2 mara baada ya kumaliza muda wake wa majaribio. Au ikiwa hatahusika na muda wa majaribio atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka amejajiriwa.

(c) Mfanyakazi ye yote ambaye hatakuwa mwanachama wa Chama kwa mujibu wa Ibara hii atakuwa ametoa taarifa yake ya kuacha kazi.

10. Malipo ya kushikia kazi kwa muda:

Mfanyakazi anapohitajiwa na Tajiri wake kushikia kwa muda kazi yenye madaraka na mshahara mkubwa zaidi kuliko wake na ikiwa kupitana huku kwa mshahara ni kwa kiasi kisichopungua Sh. 100/- kwa mwezi, na iwapo atafanya kazi hiyo kwa muda wa zaidi ya wiki moja, italazimu Tajiri amlipe licha ya mshahara wake wa kawaida, sehemu yote ya mshahara wa kazi hiyo iliyoziid mshahara wake.

11. Nguo za kazi:

(a) Wafanyakazi wenye daraja hizi zifuatazo hapa chini watapewa jozi mbili za nguo kwa mwaka:—

1. Driver.
2. Conductor.
3. Turnboys.

(b) Wafanyakazi wote ambao wamepewa nguo za kuhifadhi mwili itawalazimu kuzivaa katika nyakati zote za saa za kazi.

12. Ada za NUTA:

Imekubaliwa kwamba Tajiri atakuwa anakata ada za NUTA kila mwezi kutokana na mshahara wa kila mfanyakazi ambaye ni mwanachama wa NUTA na kuzituma pesa hizo katika Ofisi ya NUTA, Mwanza.

13. Marupurupu:

Mambo yote yaliyotajwa hapa chini yatalipwa na Tajiri kwa mujibu wa "Sheria ya Marupurupu ya 1968":—

- (1) Likizo ya mwaka na malipo yake.
- (2) Likizo ya Uzazi.
- (3) Likizo ya Ugojwa na malipo yake.
- (4) Likizo ya Ugonjwa wa Uzazi na malipo yake.
- (5) Likizo ya dharura.
- (6) Malipo ya safari ya likizo.

14. Mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba wafanyakazi wana-stahili kupewa mafunzo zaidi juu ya kazi yao ili waweze kutoa utumishi bara zaidi. Kwa ajili hiyo Tajiri ataweka mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi.

(b) Tajiri atatoa ruhusa bila ya kikwazo cho chote kwa mfanyakazi/wafanyakazi wakati wa saa za kazi inapohitajiwa, ili wadhurie mafunzo ambayo mara kwa mara hutayarishwa na Chama, au Shirika lo lote la Taifa au vyo vnginevyo.

15. Matibabu:

Tajiri atatoa cheti kwa wafanyakazi ili waweze kupata matibabu katika Hospitali ya Serikali.

16. Migogoro kazini:

(i) Migogoro yote itakayotokea kazini, kati ya Tajiri na mfanyakazi kazini ambayo inaweza kushughulikiwa chini ya Sheria ya Usalama Kazini Na. 62 ya mwaka 1964, basi Sheria hiyo itatumiwa kuondoa migogoro hiyo.

(ii) Migogoro au mabishano mengine ambayo hayaji chini ya Sheria Namba 62 ya Usalama Kazini ya mwaka 1964, usuluhishi wake utashughulikiwa kwanza kiwandani, baina ya Kamati ya Kazi kama ipo na Tajiri ili kufikia uelewano. Iwapo hatua hiyo haitafaulu mgogoro huo utapelekwa kwa Chama kwa kufuata ngazi zake. Ikiwa bado usuluhishi haujapatikana mgogoro huo utafuata Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi, 1967.

17. Mpango w kukuza mazao:

Chama na Tajiri wamekubaliana kwamba watawafunza wafanyakazi wote juu ya haja na faida ya kukuza utumishi bora na mengine kazini, na kuweka mipango mbali mbali itakayoonekana kuwa itafaa ya kukuza utumishi bora.

18. Posho ya safari:

Ikiwa mfanyakazi atasafiri kwa muda tu kwenda kazini mahali pengine mbali ya pale mahali pake pa kawaida anapofanya kazi, atalipwa posho ya safari kama hivi ifuatavyo:—

Ikiwa safari na kazi hiyo ni kutoka asubuhi mpaka jioni posho itakuwa Sh. 7/- Dereva, na Conductor Sh. 5/-, Turnboy Sh. 4/-.

19. Nyongeza ya mishahara:

Imekubaliwa ya kwamba, ili kuleta uelewano mzuri kazini na kuweka misingi ya daraja (grades) ulio mzuri nyongeza zita-tolewa kama ifuatavyo:—

(i) Conductors 2 wanaopata mshahara wa Sh. 175/- wataongezwa Sh. 9/- kila mtu.

(ii) Turnboys wanaopata mshahara wa Sh. 165/- wataongezwa Sh. 7/- kila mtu.

Mkataba huu umetiwa sahihi siku ya Ijumaa tarehe 10 Septemba, 1971.

Kwa niaba ya:

Messrs. Simu ya Upepo Bus Service

Kwa niaba ya:

Chama cha Taifa cha

Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

Haji SADIKI
Manager

M. K. J. MATOKE,
Katibu wa Mkoa

J. C. M. MANGO'NDI,
Katibu wa Tawi

R. M. ROBERT,
Mjumbe wa Wafanyakazi

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

Dar es Salaam,
26 Januari, 1972

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 440

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Hiari Na. 247 wa 1971

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA
(NUTA)

na

TANZANIA BOTTLERS LIMITED

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkataba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA) na Tanzania Bottlers Limited, uliletwa mbeie ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (b) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa ukiwa na mabadiliko yaliyokubaliwa na pande zote mbili.

Kibali hiki kitaanzia siku ya kwanza ya mwezi Januari, 1972.

MKATABA WA HIARI

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

TANZANIA BOTTLERS LIMITED.

1. Makubaliano:

Sisi tujulikanao tukiwa wote wawakilishi wa pande zote mbili tumekubaliana hali za kazi na mambo ya mishahara ifuatayo hapa chini:—

2. Muda na tarehe ya kuanza mkataba:

Mkataba huu utanzia kutoka Januari, 1972 na utaendelea kutambuliwa kwa muda wa miezi 24. Katika muda huo ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkataba huu, atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa ajili ya kusudio hilo.

Pia ikiwa ni kufuta au kubadilisha kifungu cho chote cha mkataba huu ni lazima ifuatwe masharti yaliyomo katika fasili 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal), 1967.

Hata hivyo mkataba huu utaendelea kutambuliwa mpaka wakati huo tu ambao labda mkataba utavunjwa au kubadilishwa au kurekebisha kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

3. Nyongeza:

Tumekubaliana sote kwamba nyongeza hizi zitatolewa tena kila baada ya mwaka mmoja kumalizika, kama hivi ifuatavyo:—

- (a) Wafanyakazi 71 wapatao toka Sh. 253/- hadi Sh. 499/- kwa mwezi watapata nyongeza ya Sh. 23/20 kwa mwezi.
- (b) Wafanyakazi 3 wapatao toka Sh. 500/- kwa mwezi watapata Sh. 17/- kwa mwezi.

4. Bakshishi na posho:

Tumekubaliana kwamba kwa kuwa ufanisi wa kazi umeongezeka kwa 12% Bakshishi (Bonus) itakuwa mshahara wa mwezi mmoja kwa mwaka kwa kila mfanyakazi aliyetimiza muda wa miezi isiyopungua 12.

Tumekubaliana kuwa posho itakuwa Sh. 2/- kwa kutwa kwa kila mfanyakazi, ambaye atafanya kazi kwa muda wa masaa 12 kwa ajili ya chakula.

5. Hali nyingine za kazi:

Tumekubaliana ya kama hali za kazi zilizo kwenye mkataba wetu uliopita zitaendelea kutambuliwa ila labda kuwepo na mabadiliko ya "Sheria ya Marupurupu ya mwaka 1968".

Mkataba huu umetiwa sahihi siku ya Jumatano tarehe 27 Oktoba, 1971.

Kwa niaba ya

Tanzania Bottlers Limited

G. J. INGLESSIS,
Director

D. TH. ASSEY,
Director

Kwa niaba ya

Chama cha Taifa cha
Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

B. A. MFINANGA,
Katibu wa Mkoa

J. A. MHANDO,
Katibu wa Tawi

M. S. MAMBOYA,
Katibu Msaidizi wa Tawi

BAKARI MOHAMED,
Mwenyekiti, Kamati ya Kazi

NESTOR ANTHONY,
Mwenyekiti Mdogo wa Kamati ya Kazi

Dar es Salaam,
26 Januari, 1972

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 441

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Hiari Na. 261 wa 1971

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA
(NUTA)

na

MWANZA CAPITAL HOTEL, MWANZA

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkataba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA) na Mwanza Capital Hotel, Mwanza, uliletwa mbeie ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (a) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa.

Kibali hiki kitaanzia siku wa kwanza ya mwezi Novemba, 1971.

MKATABA WA HIARI
baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

MWANZA CAPITAL HOTEL, MWANZA

1. Makubaliano:

Sisi tukiwa wawakilishi wa pande zote mbili, tumekubaliana juu ya hali na masharti ya utumishi kama ifuatavyo hapa chini:—

2. Muda na tarehe ya kuanza mkataba:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba tarehe ya kuanza mkataba huu itakuwa tarehe 1 Novemba, 1971 na utaendelea kutambuliwa kwa muda usiopungua miezi 12. Katika muda huu, ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkataba huu ni lazima afuate masharti yaliyomo katika fasili ya 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal) ya mwaka 1967.

(b) Hata hivyo mkataba unaweza kuvunjwa kwa makubaliano ya pande zote mbili, lakini ye yote katika hao anayetaka kuvunja kifungu cho chote inambidi atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa mwenzake kwa ajili ya kusudio hilo.

(c) Mkataba huu utaendelea kutambuliwa wakati wote mpaka wakati huo tu ambao labda mkataba utavunjwa, au kubadilishwa kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

3. Nyongeza za mishahara:

Tumekubaliana kuwa nyongeza za mishahara zitakuwa kama hivi ifuatavyo:—

Wafanyakazi 5 wanaopata kuanzia Sh. 169/- na zaidi wataongezwa Sh. 10/- kila mtu.

4. Masharti ya utumishi:

Tumekubaliana kuwa masharti na hali za kazi kama vilivyo katika mkataba uliopita zitaendelea kutumika, isipokuwa kama zinahusika na "Sheria ya Marupurupu ya 1968".

Mkataba huu umetiwa sahihi tarehe 24 Agosti, 1971.

Kwa niaba ya Kwa niaba ya
Mwanza Capital Hotel, Mwanza Chama cha Taifa cha
Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

D. K. RAVAL,
Mkurugenzi

M. K. J. MATOKE,
Katibu wa Mkoa

M. L. EDWARD,
Katibu Msaidizi wa Tawi

PETER MASUNGA,
Mwakilishaji wa Wafanyakazi

S. K. L. KAINDOAH,
Katibu Msaidizi

Dar es Salaam,
26 Januari, 1972

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 442

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Hiari Na. 280 wa 1971

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA
(NUTA)

na

SALUM SUUD & CO., LTD.

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkataba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tananganyika (NUTA) na Salum Suud & Co. Ltd., uliiletwa mbele ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (a) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa.

Kibali hiki kitaanzia kutoka tarehe 1 Mei, 1971.

MKATABA WA HIARI
baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

SALUM SUUD & CO., LTD.

1. Makubaliano:

Sisi Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika, tujulikanao hapa kwa jina "Chama" na Suud's Bus Service tujulikanao kwa jina "Tajiri" tumathibitisha hapa kwa maandishi na kutia sahihi zetu kuonyesha kuwa, kwa uhuru na hiari yetu wenyewe tumekubaliana juu ya mambo haya yafuatayo kuhusu hali za kazi na mishahara.

2. Utambuzi:

(a) Tajiri anakitambua na kuheshimu haki za Chama, kuwa ndiye sauti na mtetezi peke yake wa wafanyakazi wote walio wanachama wa (NUTA) kwa mambo yote yanayohusu hali za kazi na mishahara.

(b) Chama, kwa upande mwingine kinatambua Tajiri kuwa ndiye muajiri peke yake wa wafanyakazi wanaohusika na mkataba huu.

3. Kuhusika:

(a) Mkataba huu utawahusu wanachama wote wa Chama walio-iajirwa na Tajiri isipokuwa wale ambao ni wakuu wa kazi.

(b) Tafsiri ya mkuu wa kazi:

Tafsiri ya Mkuu wa kazi itakuwa na maana ifuatayo:—

- (i) Mkuu wa Kiwanda; au
- (ii) Mkuu wa Kiwanda Msaidizi; au
- (iii) Mkuu wa Idara; au
- (iv) Mkurugenzi.

Vinginevyo, Mkuu wa kazi, ni mtu ye yote yule aliyepewa madaraka na uwezo kamili kwa maandishi wa kuajiri, kufukuza, na kuachisha kazi mfanyakazi, ama uwezo wa kupendekeza juu ya kuajiri, kumfukuza, kumwachisha kazi mfanyakazi.

4. Muda na tarehe ya kuanza mkataba:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba tarehe ya kuanza mkataba huu itakuwa tarehe 1 Mei, 1971 na utaendelea kutambuliwa kwa muda wa miezi 12. Katika muda huu, ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkataba huu, ni lazima afuate masharti yaliyomo katika fasili ya 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal) ya mwaka 1967.

(b) Hata hivyo, mkataba unaweza kuvunjwa kwa makubaliano ya pande zote mbili, lakini ye yote katika hao anayetaka kuvunja kifungu cho chote inambidi atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa mwenzake kwa ajili ya kusudio hilo.

(c) Mkataba huu utaendelea kutambuliwa wakati wote mpaka wakati huo tu ambao labda mkataba utavunjwa, au kubadilishwa au kurekebisha kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

5. Kuajiri:

Muda wa majaribio utakuwa kama ifuatavyo:—

(a) Kwa kazi zisizohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya mwezi mmoja.

(b) Kwa kazi zinazohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya miezi miwili.

(c) Mara baada ya muda wa majaribio kumalizika mfanyakazi atahesabiwa kuwa ni mfanyakazi wa kudumu wa mwezi.

6. Uchaji au uachishwaji kazi:

(a) Katika muda wa majaribio upande wo wote:—

(i) Chini ya kifungu cha 5 (a) utatoa taarifa ya saa 24 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala ya taarifa hiyo.

(ii) Chini ya kifungu cha 5 (b) utatoa taarifa ya siku 14 ya kuacha au kuachishwa kazi, au malipo ya fedha badala yake.

(b) Kuhusu wafanyakazi wa kudumu, upande wo wote utatakiwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja (1) ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha ya mwezi mmoja (1) badala ya taarifa hiyo. Taarifa hiyo, au malipo badala yake ni lazima itolewe kwa maandishi.

(c) Mfanyakazi asiachishwe kazi mpaka pamekuwapo na sababu ya maana inayoambatana na uwezo au tabia yake kazini au ustawi wa kazi.

Papo hapo yafuatayo yasiwe ni sababu ya kumwachisha kazi mfanyakazi:—

(i) Kuwa mwanachama wa Chama au kufanya shughuli za Chama nje ya saa za kazi, au wakati wa saa za kazi kwa idhini ya tajiri au msimamizi wake wa kazi.

(ii) Kuwa mjumbe au Kiongozi wa wafanyakazi au kugombea kiti cho chote cha ujumbe au uongozi wa wafanyakazi.

(iii) Kutoa malalamiko au kushiriki katika utoaji wa ushahidi juu ya Tajiri kuvunja sheria, kutokufuata siasa ya Taifa au kufanya jambo lo lote la kuwaudhi wafanyakazi.

(iv) Ukabila, rangi, utu, dini, mawazo ya siasa na (Starche).

7. Nafasi za kazi na upunguzaji wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kuwa, juhudi ya pamoja itafanywa ili kuongeza nafasi za kazi na kuzuia upunguzwaji wa wafanyakazi kazini, ili kusaidia Taifa katika kupambana na tatizo la ukosefu wa kazi za mishahara nchini.

(b) Hatua za kuwapunguza idadi ya wafanyakazi, zitachukuliwa tu, iwapo Tajiri atakitoshleza Chama, kuwa hakuna uwezekano wo wote mwingine wa kuepuka au kuzuia hatua hiyo. Hizi zifuatazo zitakuwa miongoni mwa njia zifaazo kufikiriwa juu ya uepukaji wa upunguzaji wafanyakazi; uondoaji wa kazi za ziada; ubadilishaji wa wafanyakazi kutoka sehemu nyingine ambazo zitakokana kuwa na nafasi au haja na watu hao; kutoajiri tena, kwa muda watu wavya mpaka hapo hali itakapirudia tena kuwa njema; upunguzaji wa pole pole kwa wafanyakazi wote watakaohusika.

(c) Uchaguzi wa wafanyakazi watakaohusika na upunguzwaji utafuata msingi wa "Wakwanza kuingia kazini awe wa mwisho kupunguzwa" au kufikiriwa juu ya:—

(a) Haja ya utendaji bora wa kazi za kiwanda.

(b) Uwezo, uzoovu, ujuzi na sifa za kazi za kila mfanyakazi.

(c) Muda wa utumishi.

(d) Umri.

(e) Hali ya jamii yake.

(d) Wafanyakazi ambao wameachishwa kwa ajili ya upunguzaji lazima wapewe nafasi ya kwanza ya kurudishwa kazini wakati Muajiri anapojitaji wafanyakazi wavya. Kuajiriwa tena kufuate utaratibu uliyotajwa hapo juu.

8. Saa za kazi:

(a) Saa za kazi zitakuwa 45 kwa juma. Jumapili na siku za Sikukuu kwa kawaida hakutakuwa na kazi.

(b) Kazi zo zote zitakazofanyika zaidi ya saa za kazi za kawaida, kwa juma au kwa mwezi zitahesabiwa kuwa ni kazi za ziada ambayo lazima italipwa kwa kiasi cha 1½ (moja na nusu) ya malipo ya saa za kawaida. Ila tu, ikiwa kazi hizo zitafanyika siku za Jumapili au Sikukuu za Kiserikali, basi malipo yake yatakuwa mara mbili ya kiasi cha malipo ya saa za kawaida.

9. *Ulazima wa Uanachama:*

(a) Kila mfanyakazi aliyejajiwa na Tajiri atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka tarehe ya kuanza kwa mkataba huu.

(b) Mfanyakazi yote yule mpya ambaye atakayejajiwa atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi 2 mara baada ya kumalizika muda wake wa majaribio. Au ikiwa hatahusika na muda wa majaribio atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka amejajiwa.

(c) Mfanyakazi yote ambaye hatakuwa mwanachama wa Chama kwa mujibu wa Ibara hii atakuwa ametoa taarifa yake ya kuacha kazi.

10. *Nguo na au Vifaa vya kuhifadhi mwili kazini:*

(a) Wafanyakazi wenye daraja hizi zifuatazo hapa chini wata-pewa jozi mbili kwa mwaka za nguo za kuhifadhi mwili.

- (1) Madereva.
- (2) Taniboi.
- (3) Condakta.

(b) Wafanyakazi wote ambao wamepeva nguo na vifaa vya kuhifadhi mwili itawalazimu kuvifaa katika nyakati zote za saa za kazi.

11. *Ada za NUTA:*

Imekubaliwa kwamba Tajiri atakuwa anakata ada za NUTA kila mwezi kutokana na mishahara wa kila mfanyakazi ambaye ni mwanachama wa NUTA na kuzituma pesa hizo kwenye Makao Makuu ya NUTA kupitia Mahesabu Na. 1 huko katika Tawi la Benki ya Taifa ya Biashara, Mtaa wa Market, Dar es Salaam.

12. *Marupurupu:*

Mambo yote yaliyotajwa hapa chini yatalipwa na Tajiri kwa mujibu wa "Sheria ya Marupurupu ya mwaka 1968".

- (1) Likizo ya mwaka na malipo yake.
- (2) Likizo ya ugonjwa na malipo yake.
- (3) Likizo ya uzazi.
- (4) Likizo ya ugonjwa wa uzazi na malipo yake.
- (5) Likizo ya dharura.
- (6) Malipo ya safari ya likizo.

13. *Mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi:*

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba wafanyakazi wana-stahili kupewa mafunzo zaidi juu ya kazi yao, ili waweze kutoa utumishi bora zaidi. Kwa ajili hiyo Tajiri, ataweka mpango maalum wa mafunzo kwa wafanyakazi.

(b) Tajiri atatoa ruhusa bila ya kikwazo cho chote kwa wafanyakazi wakati wa saa za kazi inapohitajiwa, ili wahudhuri mafunzo ambayo mara kwa mara hutayarishwa na Chama, au Shirika lo lote la Taifa au vyo vinginevi.

14. *Matibabu:*

Kila mfanyakazi au jamaa yake anapohitaji kwenda katika matibabu tajiri atampa cheti cha matibabu.

15. *Migogoro kazini:*

(i) Migogoro yote itakayotokea kazini, kati ya Tajiri na mfanya-kazi kazini ambayo inaweza kushughulikiwa chini Sheria ya Usalama Kazini, Na. 62 ya 1964, basi Sheria hiyo itatumiwa kuondo migogoro hiyo.

(ii) Migogoro au mabishano mengine ambayo hayaji chini ya Sheria Na. 62 ya Usalama Kazini ya mwaka 1964, usuluhishi wake utashughulikiwa kwanza kirafiki, baina ya Kamati ya Kazi kama ipo, na Tajiri ili kufikia uelewano. Iwapo hatua hiyo haitafaulu mgogoro huo utapelekwa kwa Chama kwa kufuata ngazi zake. Ikiwa bado usuluhishi haujapatikana, mgogoro huo utafuata Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi, 1967.

16. *Mpango wa kukuza mazao:*

Kwa sababu kazi hii ni ya usafirishaji Chama na tajiri kitajita-hidi kila njia ili kuzuia ulalaji kazi ovyo, na kutoa huduma safi kwa abiria.

17. *Nyongeza ya mishahara:*

Imekubaliwa ya kama nyongeza za mishahara itakuwa kama hivi ifuatavyo:—

Mshahara	Nyongeza:	Wafanyakazi	Jumla
Sh. 120/-—Sh. 150/-	Sh. 14/-	3	Sh. 42/-
Sh. 151/-—Sh. 350/-	Sh. 10/-	3	Sh. 30/-
			Sh. 72/-

Mkataba huu umetiwa sahihi siku ya Ijumaa tarehe 11 Juni, 1971.

Kwa niaba ya

Salum Suud & Co. Ltd.

Chama cha Taifa cha
Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

J. B. ALMASY,

Katibu wa Tawi

Sale Proprietor

M. S. MAMBOYA,

Katibu Msaidizi wa Tawi

Katibu wa Mkoa

Mjimbe wa Wafanyakazi

Dar es Salaam,
1 Februari, 1972

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 443

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Hiari Na. 282 wa 1971

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA
(NUTA)

na

LUCK HOTEL, ARUSHA

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkataba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA) na Luck Hotel uliletwa mbele ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (a) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa.

Kibali hiki kitaanzia siku ya kwanza ya mwezi Agosti, 1971.

MKATABA WA HIARI

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

LUCK HOTEL, ARUSHA

1. *Makubaliano:*

Sisi Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika, tujulikanao hapa kwa jina "Chama" na Luck Hotel tujulikanao kwa jina "Tajiri" tunathibitisha hapa kwa maandisha na kutia sahihi zetu, kuonyesha kuwa kwa uhuru na hiari yetu wenyewe tumekubaliana juu ya mambo haya yafuatayo kuhusu hali za kazi na mishahara.

2. *Utambuzi:*

(a) Tajiri anakitambua na kuheshimu haki za Chama, kuwa ndiye sauti na mtetezi peke yake wa wafanyakazi wote walio wanachama wa NUTA kwa mambo yote yanayohusu hali za kazi na mishahara.

(b) Chama, kwa upande mwingine kinatambua Tajiri kuwa ndiye muajiri peke yake wa wafanyakazi wanaohusika na mkataba huu.

3. *Kuhusika:*

(a) Mkataba huu utawahusu wanachama wote wa Chama walio-ajiriwa na Tajiri isipokuwa wale ambao ni Wakuu wa kazi.

(b) *Tafsiri ya Mkuu wa Kazi:*

Tafsiri ya Mkuu wa Kazi itakuwa na maana ifuatavyo:—

- (i) Mkuu wa kiwanda; au
- (ii) Mkuu wa kiwanda msaidizi; au
- (iii) Mkuu wa idara; au
- (iv) Mkurugenzi.

Vinginevyo, Mkuu wa kazi, ni mtu ye yote yule aliyepewa madaraka na uwezo kamili kwa maandishi wa kuajiri, kufukuza, na kuachisha kazi mfanyakazi, ama uwezo wa kupendekeza juu ya kuajiri, kumfukuza, kumwachisha kazi mfanyakazi.

4. *Muda na tarehe ya kuanza mkataba:*

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba tarehe ya kuanza mkataba huu itakupa 1 Agosti, 1971 na utaendelea kutambuliwa kwa muda usiopungua miezi kumi na miwili. Katika muda huu, ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkataba huu, ni lazima afuate masharti yaliyomo katika fasili ya 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal) ya mwaka 1967.

(b) Hata hivyo mkataba unaweza kuvunjwa kwa makubaliano ya pande zote mbili, lakini ye yote katika hao anayetaka kuvunja kifungu cho chote inambidi atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa mwenzake kwa ajili ya kusudio hilo.

(c) Mkataba huu utaendelea kutambuliwa wakati wote mpaka wakati huo tu ambao labda mkataba utavunjwa, au kubadilishwa au kurekebisha kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

5. *Kuajiri:*

Muda wa majaribio utakuwa kama ifuatavyo:—

(a) Kwa kazi zisizohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya mwezi mmoja.

(b) Kwa kazi zinazohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya miezi miwili.

(c) Mara baada ya muda wa majaribio kumalizika mfanyakazi atahesabiwa kuwa mfanyakazi wa kudumu wa mwezi.

6. *Uchaji au uachishwaji kazi:*

(a) Katika muda wa majaribio upande wo wote:—

(i) Chini ya kifungu 5 (a) utatoa taarifa ya saa 24 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala ya taarifa hiyo.

(ii) Chini ya kifungu 5 (b) utatoa taarifa ya siku 14, ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala yake.

(b) Kuhusu wafanyakazi wa kudumu, upande wo wote utatakiwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha ya mwezi mmoja badala ya taarifa hiyo. Taarifa hiyo, au malipo badala yake, ni lazima itolewe kwa maadishi.

(c) Mfanyakazi asiachishwe kazi mpaka pamekuwapo na sababu ya maana inayoambatana na uwezo au tabia yake kazini au ustawi wa kazi.

Papo hapo yafuatayo yasiwe ni sababu ya kumwachisha kazi:—

(i) Kuwa mwanachama wa Chama au kufanya shughuli za Chama nje ya saa za kazi, au wakati wa saa za kazi kwa idhini ya Tajiri au msimamizi wake wa kazi.

(ii) Kuwa mjumbe au kiongozi wa wafanyakazi au kugombea kiti cho chote cha ujumbe au uongozi wa wafanyakazi.

(iii) Kutoa malalamiko au kushiriki katika utoaaji wa ushahidi juu ya Tajiri kuvunja Sheria, kutokufuata siasa ya Taifa au kufanya jambo lo lote la kuwaudhi wafanyakazi.

(iv) Ukabila, rangi, utu, dini, mawazo ya siasa na (Starehe).

7. *Nafasi za kazi na upunguzaji wafanyakazi:*

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kuwa, juhudi ya pamoja itafanywa ili kuongeza nafasi za kazi na kuzuia upunguzwaji wa wafanyakazi kazini, ili kusaidia Taifa katika kupambana na tatizo la ukosefu wa kazi za mishahara nchini.

(b) Hatua za kuwapunguza idadi ya wafanyakazi, zitachukuliwa tu iwapo tajiri atakitoshesha Chama, kuwa, hakuna uwezekano wo wote mwingine wa kuepuka au kuzuia hatua hiyo. Hizi zifuatazo zitakuwa miongoni mwa njia zifaazo kufikiriwa juu

ya uepakaji wa upunguzaji wafanyakazi; uondoaji wa kazi za ziada; ubadilishaji wa wafanyakazi kutoka sehemu wasikohitajiwa na kuwaweka kwenye sehemu nyingine ambazo zitaonekana kuwa na nafasi au haja na watu hao; kutoajiri tena, kwa muda wazi wapya mpaka hapo hali itakaporudia tena kuwa njema; upunguzaji wa pole pole kwa wafanyakazi wote watakaohusika.

(c) Uchaguzi wa wafanyakazi watakaohusika na upunguzaji utafuata msingi wa "Wakwanza kuingia kazini awe wa mwisho kupunguzwa" au kufikiriwa juu ya:—

- Haja ya utendaji bora wa kazi za kiwanda.
- Uwezo, uzoovu, ujuzi na sifa za kazi za kila mfanyakazi.
- Muda wa utumishi.
- Umri.
- Hali ya jamii yake.

(d) Wafanyakazi ambao wameachishwa kwa ajili ya upunguzaji lazima wapewe nafasi ya kwanza ya kurudishwa kazini wakati muajiri anapojiri wafanyakazi wapya. Kuajiriwa tena kufuate utaratibu uliotajwa hapo juu.

8. Saa za kazi:

(a) Saa za kazi zitakuwa saa 45 kwa juma. Jumapili na Siku za Sikukuu kwa kawaida hakutakuwa na kazi.

(b) Kazi zo zote zitakazofanika zaidi ya saa za kawaida kwa juma au kwa mwezi zitahesabika kuwa ni kazi za ziada ambayo lazima italipwa kwa kiasi cha 1½ (moja na nusu) ya malipo ya saa za kawaida. Ila tu, ikiwa kazi hizo zitafanyika siku za Jumapili au Sikukuu za Kiserikali, basi malipo yake yatakuwa mara mbili ya kiasi cha malipo ya saa za kawaida.

9. Ulazima wa Uanachama:

(a) Kila mfanyakazi aliyejiriwa na tajiri atalazimika kuwa mwanachama wa chama katika muda wa miezi miwili toka tarehe ya mkataba huu kutangazwa rasmi kwenye *Gazeti la Serikali*.

(b) Mfanyakazi ye yote yule mpya ambaye atakayejiriwa baada ya mkataba huu kuanza kutumika atalazimika kuwa mwanachama wa chama katika muda wa miezi 2 mara baada ya kumaliza muda wake wa majaribio. Au ikiwa hatahusika na muda wa majaribio atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka amejiriwa.

(c) Mfanyakazi ye yote ambaye hatakuwa mwanachama wa chama kwa mujibu wa Ibara hii atakuwa ametoa taarifa yake ya kuacha kazi.

10. Malipo ya kushikia kazi kwa muda:

Mfanyakazi anapohitajiwa na tajiri wake kushikia kwa muda kazi yenye madaraka na mshahara mkubwa zaidi kuliko wake na ikiwa kupitana huku kwa mshahara ni kwa kiasi kisichopungua Sh. 100/- kwa mwezi, na iwapo atafanya kazi hiyo kwa muda wa zaidi ya wiki moja, italazimu tajiri amilipe licha ya mshahara wake wa kawaida, sehemu yote ya mshahara wa kazi hiyo iliyoziidi mshahara wake.

11. Nguo za kazi:

(a) Wafanyakazi wenye daraja hizi zifuatazo hapa chini watapewa jozi mbili za nguo kwa mwaka:—

Watumishi wote wa Hoteli.

(b) Wafanyakazi wote ambao wamepewa nguo za kazi za kuhifadhi mwili itawalazimu kuzivaa katika nyakati zote za saa za kazi.

12. Ada za NUTA:

Imekubaliwa kwamba tajiri atakuwa anakata ada za NUTA kila mwezi kutokana na mshahara wa kila mfanyakazi ambaye ni mwanachama wa NUTA na kuzituma pesa hizo kwenye Makao Makuu ya NUTA kupitia Mahesabu Na. 1 huko katika Tawi la Benki ya Taifa ya Biashara, Mtaa wa Market, Dar es Salaam.

13. Marupurupu:

Mambo yote yaliyotajwa hapa chini yatalipwa na Tajiri kwa mujibu wa "Sheria ya Marupurupu ya 1968".

- Likizo ya mwaka na malipo yake.
- Likizo ya ugonjwa na malipo yake.
- Likizo ya uzazi.
- Likizo ya ugonjwa wa uzazi na malipo yake.
- Likizo ya dharura.
- Malipo ya safari ya likizo.

14. Mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba wafanyakazi wana-stahili kupewa mafunzo zaidi juu ya kazi zao ili waweze kutoa utumishi bora zaidi. Kwa ajili hiyo tajiri ataweka mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi.

(b) Tajiri atatoa ruhusa bila ya kikwazo cho chote kwa mfanyakazi/wafanyakazi wakati wa saa za kazi wanapohitajiwa, ili kuhudhuria mafunzo ambayo mara kwa mara hutayarishwa na Chama, au Shirika lo lote la Taifa au vyuo vinginevyo.

15. Matibabu:

(a) Matibabu yatatolewa bure kwa kila mfanyakazi pamoja na mkewe au mumewe na watoto wake.

(b) Kila mfanyakazi au jamaa yake anapohitaji kwenda kwenye matibabu tajiri atampa cheti cha matibabu pamoja na chambo cha kusafiria kwenda huko.

16. Migogoro kazini:

(i) Migogoro yote itakayotokea kazini, kati ya tajiri na mfanyakazi kazini ambayo inaweza kushughulikiwa chini ya Sheria ya Usalama Kazini, Na. 62 ya 1964 basi sheria hiyo itatumika kuondoa migogoro hiyo.

(ii) Migogoro au mabishano mengine ambayo hayaji chini ya Sheria Na. 62 ya Usalama Kazini ya mwaka 1964, usuluhishi wake utashughulikiwa kwanza kirafiki, baina ya Kamati ya Kazi kama ipo, na Tajiri ili kufikia uelewano. Iwapo hatua hiyo haitafaulu mgogoro huo utapelekwa kwa Chama kwa kufuata ngazi zake. Ikiwa bado usuluhishi haujapatikana, mgogoro huo utafuata Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi, 1967.

17. Mpango wa kukuza mazao:

Chama na Tajiri wamekubaliana kwamba watawafunza wafanyakazi wote juu ya haja na faida ya kukuza utumishi bora na mengine kazini, na kuweka mipango mbali mbali itakayoonekana kuwa itafaa ya kukuza utumishi bora.

18. Nyongeza ya mishahara:

Nyongeza ya mishahara itakuwa Sh. 7/- kwa kila mfanyakazi.

Kwa niaba ya
Luck Hotel, Arusha

Kwa niaba ya
Chama cha Taifa cha
Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

H. G. CHIFUPA,
Katibu wa Tawi

L. W. NGANJI,
Katibu Msaidizi wa Tawi

A. SELEMANI,
Mjumbe wa Wafanyakazi

Moshi,
18 Januari, 1972

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 444

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Hiari Na. 291 wa 1971

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

MESSRS. BRITISH TUTORIAL COLLEGE

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3 Mkataba wa Hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA) na British Tutorial College uliletwa mbele ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (a) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa.

Kibali hiki kitaanzia siku ya kwanza ya mwezi Agosti, 1971.

MKATABA WA HIARI
baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)
na

MESSRS. BRITISH TUTORIAL COLLEGE

1. Makubaliano:

Sisi Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika tujulikanao hapa kwa jina "Chama" na British Tutorial College tujulikanao kwa jina "Muajiri" tunathibitisha hapa kwa maandishi na kutia sahihi zetu, kuonyesha kuwa kwa uhuru na hiari yetu wenyewe tumekubaliana juu ya mambo haya yafuatayo kuhusu Hali za kazi na Mishahara.

2. Utambuzi:

(a) Muajiri anakitambua na kuheshimu haki za Chama, kuwa ndiye sauti na mtetezi peke yake wa wafanyakazi wote walio wanachama wa NUTA kwa mambo yote yanayohusu hali za kazi na mishahara.

(b) Chama, kwa upande mwingine kinatambua Muajiri kuwa ndiye muajiri peke yake wa wafanyakazi wanaohusika na mkataba huu.

3. Kuhusika:

(a) Mkataba huu utawahusu wanachama wote wa Chama walioajiriwa na Muajiri isipokuwa wale ambao ni Wakuu wa kazi.

(b) Tafsiri ya mkuu wa kazi:

Tafsiri ya Mkuu wa Kazi itakuwa na maana ifuatayo:—

- Mkuu wa kiwanda; au
- Mkuu wa kiwanda Msaidizi; au
- Mkuu wa Idara; au
- Mkurugenzi.

Vinginevyo, mkuu wa kazi ni mtu ye yote yule aliyepewa madaraka na uwezo kamili kwa maandishi wa kuajiri, kufukuza na kuachisha kazi mfanyakazi, ama uwezo wa kupendekeza juu ya kuajiri, kumfukuza au kumwachisha kazi mfanyakazi.

4. Muda na tarehe ya kuanza mkataba:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba tarehe ya kuanza mkataba huu itakuwa 1 Agosti, 1971 na utaendelea kutambuliwa kwa muda usiopungua miezi 12. Katika muda huu, ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkataba huu, ni lazima afuate masharti yaliyomo katika fasili ya 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal) ya mwaka 1967.

(b) Hata hivyo mkataba unaweza kuvunjwa kwa makubaliano ya pande zote mbili. Lakini ye yote katika hao anayetaka kuvunja kifungu cho chote inambidi atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa mwenzake kwa ajili ya kusudio hilo.

(c) Mkataba huu utaendelea kutambuliwa wakati wote mpaka wakati huo tu ambao labda mkataba utavunjwa, au kubadilishwa au kurekebishwa kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

5. Kuajiri:

(a) Kila mfanyakazi atakayejiriwa na British Tutorial College atakuwa katika majaribio kwa muda wa mwezi mmoja.

(b) Mara baada ya muda wa majaribio kumalizika mfanyakazi atahesabiwa kuwa ni mfanyakazi wa kudumu wa mwezi.

6. Uchaji au uachishwaji kazi:

(a) Katika muda wa majaribio upande wo wote:—

Utatoa taarifa ya saa 24 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala ya taarifa hiyo.

(b) Kuhusu wafanyakazi wa kudumu, upande wo wote utatakiwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha ya mwezi mmoja badala ya taarifa hiyo. Taarifa hiyo, au malipo badala yake, ni lazima itolewe kwa maandishi.

(c) Mfanyakazi asiachishwe kazi mpaka pamekuwapo na sababu ya maana inayoambatana na uwezo au tabia yake kazini au ustawi wa kazi.

Papo hapo yafuatayo yasiwe ni sababu ya kumwachisha kazi:—

(i) Kuwa mwanachama wa chama au kufanya shughuli za chama nje ya saa za kazi au wakati wa saa za kazi kwa idhini ya muajiri au msimamizi wake wa kazi.

(ii) Kuwa mjumbe au kiongozi wa wafanyakazi au kugombea kiti cho chote cha ujumbe au uongozi wa wafanyakazi.

(iii) Kutoa malalamiko au kushiriki katika utoaji wa ushahidi juu ya Muajiri kuvunja sheria, kutokufuata siasa ya Taifa, au kufanya jambo lo lote la kuwaudhi wafanyakazi.

(iv) Ukabila, rangi, utu, dini mawazo ya siasa na (starehe).

7. Nafasi za kazi na upunguzaji wa wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kuwa juhudi ya pamoja itafanywa ili kuongeza nafasi za kazi na kuzuia upunguzaji wa wafanyakazi kazini, ili kusaidia Taifa katika kupambana na tatizo la ukosefu wa kazi za mishahara nchini.

(b) Hatua za kuwapunguza idadi ya wafanyakazi, zitachukuliwa tu, iwapo Muajiri atakitoshesha Chama, kuwa hakuna uwezekano wo wote mwingine wa kupuka au kuzuia hatua hiyo. Hizi zifuatazo zitakuwa miongoni mwa njia zifaazo kufikiriwa juu ya uepukaji wa upunguzaji wa wafanyakazi; uondoaji wa kazi za ziada; ubadilishaji wa wafanyakazi kutoka sehemu wasikohitajika na kuwaweka kwenye sehemu nyingine ambazo zitaonekana kuwa na nafasi au haja na watu hao; kutoajiri tena, kwa muda, watu wapya mpaka hapo hali itakaporudia tena kuwa njema; upunguzaji wa pole pole kwa wafanyakazi watakoahusika.

(c) Uchaguzi wa wafanyakazi watakoahusika na upunguzaji utafuata msingi wa "Wakwanza kuingia kazini awe wa mwisho kupunguzwa" au kufikiriwa juu ya:—

(a) Haja ya utendaji bora wa kazi za kiwanda.

(b) Uwezo, uzoovu, ujuzi na sifa za kazi za kila mfanyakazi.

(c) Muda wa utumishi.

(d) Umri.

(e) Hali ya jamii yake.

(d) Wafanyakazi ambao wameachishwa kazi kwa ajili ya upunguzaji lazima wapewe nafasi ya kwanza ya kurudishwa kazini wakati muajiri anapojiri wafanyakazi wapya. Kuajiriwa tena kufuata utaratibu uliotajwa hapo juu.

8. Saa za kazi:

(a) Saa za kazi zitakuwa 39 kwa juma. Jumapili na siku za sikukuu kwa kawaida hakutakuwa na kazi.

(b) Kazi zo zote zitakazofanyika zaidi ya saa za kawaida, kwa juma au kwa mwezi zitahesabika kuwa ni kazi za ziada ambayo lazima italipwa kwa kiasi cha 1½ (moja na nusu) ya malipo ya saa za kawaida. Ila tu ikiwa kazi hizo zitafanyika siku za Jumapili au sikukuu za Kiserikali basi malipo yake yatakuwa mara mbili ya kiasi cha malipo ya saa za kawaida.

9. Ulazima wa Uanachama:

(a) Kila mfanyakazi aliyejiriwa na Messrs. British Tutorial College atalazimika kuwa mwanachama wa NUTA katika muda wa miezi miwili toka tarehe ya mkataba huu utakapotangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali.

(b) Mfanyakazi yo yote yule mpya ambaye atakayejiriwa atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili mara baada ya kumaliza muda wake wa majaribio. Au ikiwa hatahusika kwa muda wa majaribio atalazimika kuwa mwanachama wa chama katika muda wa miezi miwili toka amejiriwa.

(c) Mfanyakazi ye yote ambaye hatakuwa mwanachama wa chama kwa mujibu wa Ibara hii atakuwa ametoa taarifa yake ya kuacha kazi.

10. Nguo na au vifaa vya kuhifadhi mwili kazini:

Imekubaliwa kuwa:—

(a) Tarishi wa ofisi atapewa jozi mbili za nguo kwa mwaka.

(b) Nguo ambazo atapewa itamlazimu kuzivaa katika nyakati zote za saa za kazi.

11. Ada za NUTA:

Imekubaliwa kwamba Muajiri atakuwa anakata ada za NUTA kila mwezi kutokana na mishahara wa kila mfanyakazi ambaye ni mwanachama wa NUTA na kuzituma pesa hizo kwenye Makao Makuu ya NUTA kupitia Mahesabu No. 1 huko katika Tawi la Benki ya Taifa ya Biashara, Mtaa wa Market, Dar es Salaam.

12. Marupurupu:

Mambo yote yaliyotajwa hapa chini yatalipwa na Muajiri kwa mujibu wa "Sheria ya Marupurupu ya 1968".

(1) Likizo ya mwaka na malipo yake.

(2) Likizo ya ugonjwa na malipo yake.

(3) Likizo ya uzazi na malipo yake.

(4) Likizo ya ugonjwa wa uzazi na malipo yake.

(5) Likizo ya dharaura; na

(6) Malipo ya safari ya likizo.

13. Mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi:

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba wafanyakazi wana-stahili kupewa mafunzo zaidi juu ya kazi zao ili waweze kutoa utumishi bora zaidi. Kwa ajili hiyo Muajiri, ataweka mpango maalum wa mafunzo kwa wafanyakazi.

(b) Muajiri atatoa ruhusa bila ya kikwazo cho chote kwa wafanyakazi, wakati wa saa za kazi anapohitajwa, ili wahudurie mafunzo ambayo mara kwa mara hutayarishwa na Chama, au Shirika lo lote la Taifa au vyuo vinginevyo.

14. Chakula kazini:

Imekubaliwa kwamba ili kuwezesha wafanyakazi waweze kutoa utumishi bora kazini, Muajiri atatoa chai mara mbili kwa kutwa kwa wafanyakazi pamoja na vifaa. Gharama zote zitalipwa na Muajiri, Muajiri atashirikiana na wafanyakazi kuweka utaratibu wa kufaa juu ya saa za kunywa na mambo mengineo kuhusu namna ya utoaji wa chai hiyo.

15. Matibabu:

Kila mfanyakazi anapohitaji kwenda katika matibabu Muajiri atampa cheti cha matibabu. Katika hospitali au Dispensary ya Serikali.

16. Migogoro kazini:

(i) Migogoro yote itakayotokea kazini kati ya Muajiri na mfanyakazi kazini ambayo inaweza kushughulikiwa chini ya Sheria ya Usalama Kazini Namba 62 ya 1964 basi sheria hiyo itatumiwa kuondoa migogoro hiyo.

(ii) Migogoro au mabishano mengine ambayo hayaji chini ya Sheria Nambari 62 ya Usalama Kazini ya mwaka 1964, usuluhishi wake utashughulikiwa kwanza kirafiki, baina ya Kamati ya Kazi kama ipo, na tajiri ili kufikia ulewano. Iwapo hatua hiyo haitafaulu mgogoro huo utapelekwa kwa Chama kwa kufuata ngazi zake. Ikiwa bado usuluhishi haujapatikana, mgogoro huo utafuata Sheria ya Baraza la Kudumu la Wafanyakazi, 1967.

17. Nyongeza za mishahara:

Imekubaliwa ya kama nyongez za mishahara itakuwa kama hivi ifuatavyo:—

Kundi	Mshahara	Watu	Nyongeza	Jumla
I	Sh. 306/-—Sh. 355/-	4	Sh. 26/-	Sh. 104/-
II	Sh. 511/-—Sh. 576/-	2	Sh. 17/-	Sh. 34/-

Mkataba huu umetiwa sahihi siku ya Jummosi Septemba, tarehe 11 mwaka 1971.

Kwa niaba ya

British Tutorial College

Kwa niaba ya

Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

B. A. MFINANGA,
Katibu wa Mkoa

J. B. ALMASY,
Katibu wa Tawi

R. B. K. SHUMAH,
Katibu Msaidizi wa Tawi

Dar es Salaam,
1 Februari, 1972

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 445

LD. 64640

UBATILISHO WA HAKI YA KUMILIKI ARDHI

Hati ya Haki ya kumiliki Kiwanja, yenye Land Office No. 25038, Certificate of Title No. 18181 juu ya Kiwanja Na. 4 na 5, Kitalu "H", Mjini Songea, vilivyomilikiwa na PANAYIOTTIS APOSTOLOU *SOUTIS ilibatilishwa kwa mamlaka ya Mtukufu Rais mnamo tarehe 15 mwezi Februari, 1972.

Dar es Salaam,
7 Machi, 1972

K. S. K. LUGAKINGIRA,
Kaimu Kamishna wa Ardhi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 446

LD. 64640

UBATILISHO WA HAKI YA KUMILIKI ARDHI

Hati ya Haki ya kumiliki Kiwanja, yenye Land Office No. 25039, Certificate of Title No. 18180 juu ya Kiwanja Na. 6, Kitalu "H", Mjini Songea kilichomilikiwa na COSTAS NICOLAOU PAPADIMITRIOU ilibatilishwa kwa mamlaka ya Mtukufu Rais mnamo tarehe 15 mwezi Februari, 1972.

Dar es Salaam,
7 Machi, 1972

K. S. K. LUGAKINGIRA,
Kaimu Kamishna wa Ardhi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 447

LD. 62719

UBATILISHO WA HAKI YA KUMILIKI ARDHI

Hati ya Haki ya kumiliki Ardhi yenye Land Office No. 23885, Certificate of Title No. 17166 juu ya Kiwanja Na. 1, Block 37 "A", Kinondoni Area, Mjini Dar es Salaam, ambayo ilimilikiwa na ABEL SAFARI JOSEPH MALEMA, ilibatilishwa kwa amri ya Mtukufu Rais mnamo tarehe 4 mwezi Januari, 1972.

Dar es Salaam,
24 Februari, 1972

K. S. K. LUGAKINGIRA,
Kaimu Kamishna wa Ardhi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 448

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI

Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
(Sura ya 334)

Hati Nambari: 186099/45.

Mmiliki aliyeandikishwa: WAZIRI JUMA WAZIRI.

Ardhi: Plot No. 4, L.O. No. 22801, Kurasini West, Dar es Salaam.
Eneo: 33,400 Square feet.

Taarifa imetolewa kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa juu imepotea na ninakusudia kutoa hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii.

Hati ya asili ikionekana, lazima irudishwe kwa Msajili wa Hati, Idara ya Hati za Ardhi, S.L.P. 1191, Dar es Salaam, au kwa Kamishna wa Wilaya.

Dar es Salaam,
8 Machi, 1972

S. M. DAYA,
Msajili wa Hati Msaidizi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 449

KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA KWA NDEGE
(GOVT. AIR WARRANT)

SERIAL No. 62051-62075

Kitabu hiki kikiwa katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Lindi na ambacho kilikuwa bado hakijawahi kutumika kimepotea mnamo mwezi Januari, 1972.

Kuanzia mwezi kitabu hiki kilipopotea, matumizi yake sio halali kwa hiyo mwananchi ye yote anayejua au kupata fununu kuhusu kitabu hiki anaombwa atoe habari katika kituo cha Polisi cha karibu yake au amfahamisha Katibu Tawala wa Mkoa, Lindi haraka iwezekanavyo.

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S.L.P. 1054,
Lindi,
1 Machi, 1972

M. T. MTOTA,
Katibu Tawala

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 450

KUPOTEA KWA WARANTI ZA KUSAFIRIA
(Motor Traffic)

